EAST AFRICANA COLLECTION

# SANAA KATIKA TAFSIRI: MATATIZO NA ATHARI ZAKE

**EDITH KATHOKI MUTIE**

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA M.A. KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

**1997**

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146619 2

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

## YALIYOMO

Ukurasa


Ungamo ..... iii
Tabaruku ..... iv
Shukrani ..... v
Muhtasari ..... vii

SURA YA KWANZA
- Utangulizi ..... 1
- Somo la Utafiti ..... 3
- Madhumuni ya Tasnifu ..... 5
- Sababu za kuchagua somo ..... 6
- Haipothesia ..... 9
- Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ..... 9
- Upeo wa Tasnifu ..... 13
- Msingi wa kinadharia ..... 14
- Njia za utafiti ..... 17
- Tanbihi ..... 18

SURA YA PILI
- Utangulizi ..... 19
- Dhana za Tafsiri ..... 19
- Uhusiano wa matatizo ya tafsiri na sanaa ..... 22
- Tatizo la ukosefu wa nadharia ..... 22
- Sanaa na umbuji katika tafsiri ..... 24
- Matatizo ya kiisimu ..... 27
- Tatizo la kimawasiliano ..... 30
- Tatizo la kimaana ..... 31
- Matatizo ya kitamaduni na kimazingira ..... 33
- Matatizo ya kifani ..... 34
- Hitimisho ..... 36
- Tanbihi ..... 37

SURA YA TATU
- Utangulizi ..... 39
- Uhakiki wa Mizigo ..... 39
- Tafsiri ya lugha ya kishairi ..... 40
- Tafsiri za kitamathali ..... 51
- Tafsiri ya methali ..... 52
- Tafsiri za nahau ..... 56
- Tafsiri za moja kwa moja ..... 59
- Umbuji wa mwandishi katika tafsiri ..... 64
- Tafsiri za sitiari na tashbiha ..... 68
- Hitimisho ..... 72
- Tanbihi ..... 73

SURA YA NNE
- Hitimisho ..... 74

MAREJELEO ..... 77

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya M.A. katika chuo kingine.

**Edith K. Mutie**
(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kwa mtihani kwa idhini yetu sisi tulioteuliwa kuisimamia

4/9/97

**Bw. Michira**
(Msimamizi)

**Bi. Rose Shake**
(Msimamizi)

## KUTABARUKU

*Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu. Baba Lucas Mutie ambaye hakuishi kuona matunda ya juhudi zake na mama Magdalene Mbete kwa Maadili na wema wake usio kifani. Sijui cha kukupa iwe yako fidia.*

## SHUKRANI

Shukrani zangu nazitoa kwa wote walioniongoza katika kuitayarisha kazi hii. Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Isimu na lugha za Kiafrika wa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa mawaidha na ushauri wao.

Ningependa kutoa shukrani maalumu kwa wasimamizi wangu Bw. Michira na Bi. Rose Shake. Ushirika na uhakiki wao wa maoni yangu ndio uliwezesha kufaulu kwa kazi hii. Hawakuchoka na kusoma na kukosoa kazi yangu mara kwa mara,kwa uvumilivu wao, nasema shukrani. Nawaombea kila la kheri katika kila watakalolitenda.

Nawashukuru mama mzazi Bi. Magdalene Mbete ambaye alikuwa yupo kila nilipomhitaji. Nawashukuru ndugu zangu wote kwa kunihimiza kila nilipolemewa.

Wenzangu wote ambao tulishirikiana katika kuitafuta shahada ya M.A.nawashukuru. Tom Olali, Osano Omondi, Waithera Karis, Hannington Kilelu, Donald osiemo, Nyamberison na Du Shung Fang ambaye alirudi kwao na kutuacha katikati ya safari. Wote nawapa moyo wa shime. Kwako Omondi, "tulishirikiana" kwa mengi.! Nakushukuru.

Shukrani za dhati na za moyo wangu wote ni kwa Bw. K.F. Pocock ambaye namuwia shukrani za kipekee. Usaidizi wake katika lugha na somo alilofahamu kidogo kulihusu haukuwa na kipimo. Bila wewe singeweza chochote. Mapenzi yako ya dhati yananifanya kuhisi kuwa fahari inayotokana na shahada hii ni yetu sote. *You were always there. You always put a smile on my face after the day's tedious toil, and moil, you and our lovely little*

*Loldia Drummer Boy. Thank you for all - through it all.*

Nakishukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunipatia nafasi ya kuisomea shahada hii. Naishukuru hazina ya Gandhi Smarak Nidhi kwa kugharamia masomo yangu. Shukrani za dhati ni kwa Bw. Mutangili kwa mchango wake ambao mwenyewe aufahamu.

Kwa kuhitimisha, nawashukuru Bw. na Bi. Kyule kwa kujitolea kuipiga chapa kazi hii: Mungu na awabariki nyote.

# MUHTASARI

Kazi nyingi za tafsiri hudhamiria kuiboresha tafsiri na athari zake katika Kiswahili; ikizingatia matatizo, makosa, dosari na athari zake juu ya fasihi kwa jumla.

Uhakiki huu umejikita katika kazi moja ya kifasihi ambayo imetafsiriwa katika Kiswahili, *Mizigo*, (1977) iliyofanywa na Bi. A. Muro. Tuliangalia kazi hii tafsiri huku tukiilinganisha na kazi asilia, *The Burdens* ya John Ruganda kwa kuchunguza athari za mtindo katika tafsiri. Tulifanya hivi kwa sababu tuliamini ya kuwa dosari zilizoko katika kazi hii zinajitokeza pia katika kazi zote za fasihi tafsiri.

Ni jambo lisilowezekana kuziangalia kazi zote za tafsiri zilizoko katika Kiswahili. Kazi hii tunatumaini ya kuwa itakuwa kielelezo cha yanayohusika katika kitendo cha kutafsiri kazi nyengine za aina hii.

Tafsiri hii imegawika katika sura nne, kila moja ikijadili kipengele maalumu juu ya kitendo cha kutafsiri kwa mujibu wa fasihi. Kila sura ina hitimisho ambapo maoni na msimamo wa tasnifu hii umetolewa kwa mujibu wa yanayojitokeza katika utafiti.

Sura ya kwanza ni utangulizi unaobainisha kiini cha utafiti kuhusu sanaa katika tafsiri. Katika sura hii tumeangaza umuhimu wa kufanya uchunguzi kuhusu kitendo cha kutafsiri. Kuna pia madhumuni, misingi ya nadharia, upeo wa tasnifu, sababu za kuchagua somo na jinsi utafiti utakavyofanywa.

Sura ya pili inajadili matatizo ya tafsiri kwa jumla na jinsi yanavyochangia katika kupotoka kwa sanaa katika tafsiri. Inaangalia dhana ya tafsiri na kufafanua pamoja na kujadili athari za kila mojawapo ya matatizo hayo kwa sanaa ya makala pokezi. Haya yote yamefanywa kwa ajili ya kuweka misingi thabiti na bora ya uhakiki wa kazi iliyoteuliwa.

Sura ya tatu ni uhakiki halisi wa makosa ya kisanaa katika kazi ya *Mizigo*. Katika sura hii, uhakiki umefanywa kwa mujibu wa misingi ya kinadharia iliyojadiliwa katika sura iliyotangulia. Dosari mbalimbali za kisanaa zinazijitokeza zimetajwa, hali kadhalika matatizo yaliyomkabili mtafsiri. Mambo hayo yote yamechukuliwa mifano tu ya kuangazia uhalisi wa fasihi tafsiri kwa jumla.

Sura ya nne ni hitimisho inayotoa muhtasari wa maoni kutokana na utafiti. Maoni ya jumla, mapendekezo ya utafiti mpya na msimamo wa tasnifu umebainishwa.

# SURA YA KWANZA

## 1:1 UTANGULIZI

Somo la tafsiri sio jambo geni kwa wasomi kwani limewahi kushughulikiwa katika nyanja mbalimbali hapo awali. Wasomi na wataalamu wengi wameishughulikia tafsiri kwa madhumuni na dhamira mbalimbali. Kulishughulikia kwetu somo hili kunalenga tafsiri ya tamthilia hususani tamthilia ya John Ruganda *The Burdens* na kufaulu au kutofaulu kwa tafsiri yake *Mizigo* (1977) iliyofanywa na Bi. A. Muro.

Ijapokuwa mtafsiri hunuia kuwasilisha ujumbe, hutokea nyakati ambapo ujumbe ulionuiwa hautimiki na hata ukitimika si jinsi ulivyotimizwa katika makala asilia. Haya hutokana na sababu ya jumla ya vipengele kama vile tofauti za tamaduni, mazingira, ukwasi wa lugha kwa upande wa mtafsiri, n.k.

Tutajishughulisha hasa na kuchunguza ni kwa kiwango kipi lugha inaathirika kisanaa katika tafsiri. Mara nyingi kazi za tafsiri huwa zimenyimwa pumzi za uhai kwa kung'olewa sanaa yake na kuachwa zikiyumbayumba hewani[1]. Mtokeo yake huwa ni kwamba kazi tafsiri huwa haina ule mnato na ladha inayopatikana katika kazi asilia.

Dhana ya tafsiri ina historia yake. Kama tujuavyo, fasihi yoyote hufungamana na maendeleo ya jamii katika kipindi maalumu cha historia. Historia hiyo sisi hatutaiingilia kwa undani lakini tutataja kwamba, ni kupitia kwa tafsiri hizi ambapo athari za kimaudhui na kimtindo ziliingia katika fasihi ya Kiswahili na baadaye kuathiri watunzi wa Kiswahili.

Fasihi ya Kiswahili imekuwa ikibadilika kadiri jamii yake ilivyobadilika. Maingiliano ya kabila za Waswahili na Wazungu wakoloni yaliathiri fasihi ya Kiswahili na pia kuendeleza tafsiri. Wakati huo baadhi ya hao wakoloni waliandika hadithi na habari za Kiswahili na nyingine ambazo hapo awali ziliandikwa kwa Kiingereza zilitasiriwa. Baada ya ukoloni, Wazungu kama vile L. Krapf na Askofu Steere walitoa fasiri za kwanza za vifungu vya Biblia.

Katika fasihi, utanzu wa riwaya na utanzu wa tamthilia umefanyiwa tafsiri kuliko utanzu wa ushairi. Hata hivyo, tanzu za ushairi na riwaya zimefanyiwa utafiti kuliko utanzu wa tamthilia. Ari ya kufanya utafiti huu imetokana na ufahamu kwamba tafsiri ya tamthilia bado haijafanyiwa utafiti wa kutosha.

Ni kweli kwamba tafsiri zimetoa mchango mkubwa katika kupanua fasihi ya Kiswahili. Zimesaidia kuvusha lugha nyingine hadi Kiswahili ambapo kazi hizo zimeundwa na kupatiwa msisimuo wa kimtindo na kimaudhui unaotokana na fasihi nyingine. Kuingia kwa kazi za tafsiri katika fasihi ya Kiswahili kumezusha mijadala mingi baina ya wanaolipinga jambo hili na wale wanaolikubali. Sisi hatutachangia katika mjadala huu. Dai kwamba kazi tafsiri ni dhaifu zikilinganishwa na kazi asilia halipingiki[2].

Inadaiwa pia kwamba, vitabu vilivyotafsiriwa hadi lugha ya Kiswahili vinaiua fasihi ya Kiswahili badala ya kuiendeleza. Wasomaji wa tafsiri hizo za fasihi iliyoandikwa asilia kwa lugha nyingine huwa hawaoni mnato wala ladha yoyote ya kisanaa kwenye kazi hizo. Nyingi za kazi tafsiri huwa na lugha ya kiwango cha chini. Kazi hizo pia huwa hazina ufasaha kama lugha katika tungo asilia. Kwa sababu hii, maudhui ya tafsiri hayaendelezwi vyema au ujumbe unaowakilishwa mara nyingi unapotea. Kunatokea ukosefu wa uthabiti katika uwasilishaji wa

ujumbe asilia kwenye tafsiri.

Tutachunguza na kutazama udhaifu unaosababishwa na kupotea kwa sanaa katika kazi tafsiri. Kupamba kwa lugha kwa mwandishi ndiyo sanaa yake. Ikiwa kazi tafsiri itatumia lugha ambayo si sahihi au kutumia lugha tofauti na ya kazi asilia, basi itaathiri fani ya kazi asilia, na hatimaye maudhui ya kazi asilia kwa jumla. Matokeo yake ni kwamba, kazi tafsiri haitapendeza kisanaa[3].

Tunakubaliana na dai kwamba Kiswahili kimepokea kazi nyingi za tafsiri ambazo kwa kiwango kikubwa zimekuza fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo udhaifu unaosababishwa na tafsiri hizo hauna budi kuchunguzwa na kuonyeshwa.

**1:2 SOMO LA UTAFITI:**

Chambilecho Newmark (1988), kuwepo kwa dosari za aina mbalimbali ni jambo linalotarajiwa katika tafsiri yoyote. Anasema,

> "...hakuna kitu kama tafsiri iliyokamilika, ni ustadi ambao huhitaji lugha mwafaka na matumizi yanayokubalika"[4] (tafsiri yetu).

Ingawa watafsiri hujitahidi kuepuka matatizo mengi yanayokumba tafsiri, dosari kama vile upotoshi wa maana, sarufi ya lugha pokezi na udhaifu wa fasaha ya lugha hujitokeza kila mara katika fasihi tafsiri. Haya husababisha tafsiri kuwa za kiwango cha chini, hali ambayo inaweza kurekebishwa hivi kuziboresha kazi hizo zaidi. Kuboreshwa kwa kazi tafsiri kwa kuzitathmini, kuzikosoa na kuzichanganua kutazuia tafsiri duni. Tafsiri huwa na jukumu la kuwasilisha ujumbe wa mtu mwingine kwa hadhira inayotumia lugha tofauti na ile iliyotumiwa na mwandishi asilia. Kusisitiza haya, Brower anasema,

> "Jukumu kuu la watafsiri wote ni kujaribu kuunda kisawe cha hali ya makala asilia. Mtafsiri ni mbunifu na kama mwandishi asilia anapanga na kueleza matukio katika matamshi yaliyo na utaratibu fulani wa kiutendaji"[5].

Kazi nyingi nzuri za kifasihi kutoka tamaduni nyingine za ulimwengu zimefika katika Kiswahili zikiwa zimefinywa na kupotoshwa kifani, kimaudhui na kimaana. Sanaa ya kazi yoyote huathirika pale tu fani inapoathirika.

Somo la utafiti wetu litakuwa juu ya tamthilia zilizotafsiriwa. Tutajikita katika tamthilia ya John Ruganda *The Burdens* na makala tafsiri *Mizigo* iliyotafsiriwa na Bi A. Muro. Tutalinganisha makala asilia na makala tafsiri na kuchunguza ni kwa kiwango kipi tafsiri hiyo imefaulu.

Baada ya kusoma na kuhakiki tamthilia ya *The Burdens* ya John Ruganda, tumeona kwamba kuna mambo chungu nzima ambayo hayakuwasilishwa vilivyo katika kazi tafsiri *Mizigo* iliyofanywa na Bi. A. Muro. Ule ukwasi wa lugha na matumizi ya fani kisanaa yanayojitokeza katika *The Burdens* yamejitokeza kwa njia tofauti sana katika makala tafsiri *Mizigo*. Uzito wa maudhui, matumizi ya lugha kitamathali na ushairi katika *The Burdens* vile vile haupo katika tafsiri yake *Mizigo*.

Katika somo letu la utafiti, tutamulika katika sehemu mbili kuu, fani na maudhui. Kwa upande wa fani tutachunguza ikiwa je, ushairi ulio katika *The Burdens* kama vile,

VOTE VALOUR
VOTE VALUE
VOTE VINCENT[6]

ni tofauti na ule tunaopata katika kazi tafsiri. Vilevile, mbinu alizotumia John Ruganda kama

vile methali, jazanda na tashbiha zimejitokezaje katika kazi tafsiri? Wahusika wanaopatikana katika tafsiri ndio walewale tunaowapata katika makala asilia? Maudhui Je? Uzito wa mizigo inayozungumziwa katika *The Burdens* ni sawa na ule wa mizigo inayopatikana katika kazi tafsiri?

Baada ya kuzisoma na kuzilinganisha kazi hizi, yaani kazi asilia ya *The Burdens* na kazi tafsiri ya *Mizigo*, tumeona kwamba matumizi ya lugha katika kazi asilia yana ufasaha mwingi ilhali sanaa imedhoofishwa katika kazi tafsiri. Kwa sababu hii, tunaona kwamba ipo haja ya kuonyesha tofauti hizi zinazojitokeza katika kazi tafsiri kwa kuilinganisha kazi asilia na kazi tafsiri. Baadaye tutaweza kueleza kuweko kwa tofauti hizi na kuonyesha lugha ambayo ingetumika pale ambapo itatubidi.

**1:3 MADHUMUNI YA TASNIFU**:

Katika sehemu iliyotangulia, tumetaja kwamba kazi tafsiri ya *Mizigo* ni dhaifu ikilinganishwa na kazi asilia *The Burdens*. Madhumuni ya tasnifu yetu ni kuonyesha udhaifu huo hasa kwa upande wa fani na maudhui. Tutaonyesha kwa kutoa mifano, athari za udhaifu wa fasihi ya Kiswahili. Tutaangalia haya kwa sababu tunaamini kwamba tafsiri yenye dosari au tafsiri dhaifu haiwezi kufikisha katika Kiswahili faida na manufaa tunayotarajia kutoka kazi za tafsiri. Ni kweli kwamba hakuna tafsiri iliyokamilika lakini mtafsiri huhitajika kujitolea mhanga na kujitokeza na kazi inayokaribiana sana na kazi asilia. Ili kuendeleza fasihi ya Kiswahili kutokana na mchango wa tafsiri, tutahitajika kuwa na tafsiri nzuri.

Swali kuu ambalo tasnifu hii itajaribu kujibu kuhusu tafsiri ni je, kupotea kwa sanaa katika kazi tafsiri kunaweza kuathiri tafsiri kwa kiwango kipi? Kujibu swali hili, tasnifu itajaribu

kuonyeasha namna kupotea kwa sanaa au kudhoofishwa kwake kunavyoweza kuathiri maudhui na ladha ya kazi tafsiri kwa jumla. Makosa tutakayoonyesha na kujadili katika kazi tafsiri ya *Mizigo* yatakuwa idhibati na dhihirisho ya makosa yanayotokea katika tafsiri kwa jumla. Kazi hii itakuwa ni mfano tu wa kuonyesha udhaifu uliopo katika tafsiri nyingine.

Mtafsiri wa kazi tafsiri ya *Mizigo* ameyaondoa makali yanayojitokeza katika kazi asilia *The Burdens* ambayo bila shaka yaliwekwa hapo kwa sababu maalumu. Matokeo yake ni kwamba kazi tafsiri ya *Mizigo* imejitokeza kuwa na lugha dhaifu ikilinganishwa na kazi asilia *The Burdens* jambo ambalo limeathiri tamthilia yote kwa jumla. Ni matumaini yetu kwamba tasnifu yetu itakuwa imechangia katika jumla ya kazi zote za fasihi tafsiri zilizokwisha kupokewa katika Kiswahili.

**1:4 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO:**

Tafsiri ina umuhimu wake katika mawasiliano baina ya watu wa tamaduni mbalimbali za ulimwengu. Umuhimu wa mawasiliano hayo kwa kutumia Kiswahili unazidi kukua kutokana na kuongezeka kwa maingiliano baina ya watu kutoka katika sehemu tofauti katika maeneo kinamozungumzwa Kiswahili. Ni kutokana na tafsiri ambapo lugha za kilimwengu zimepata kunufaika na kuinua viwango vya hali zao.

Kwa upande mwingine, tafsiri haijapewa umuhimu kama taaluma maalumu katika vyuo vingi. Kumekuwa na kuongezeka kwa makala tafsiri ya aina mbalimbali bila taaluma hii yenyewe kupewa hadhi kiusomi[7]. Tunatumaini kwamba tasnifu hii itachangia katika kuendeleza taaluma hii kiusomi. Vilevile, ingawa tunakubaliana na dai kwamba vitabu vya Kiswahili vilvyotafsiriwa vina dosari, utafiti bado haujafanywa kuhusu kinachosababisha dosari hizi. P.

Newmark (1988) anasema,

> "Sababu kuu ya kutafsiri mchezo ni kuufanya uigizwe vyema. Kwa sababu hii, mtafsiri wa drama hana budi kutilia maanani hadhira. Mtafsiri hawezi kutafsiri mambo ya kitamaduni katika lugha asilia. Mtafsiri wa drama anapaswa kutumia maneno kimkato, sio afanye zaidi ya kutafsiri"[8] (tafsiri yetu)

Mtafsiri wa drama ni sharti pia alenge lugha inavyotumika wakati huo ikiwa anataka mhusika wake "aishi". Tofauti za kitabaka, daraja la elimu na uana wa mhusika ni lazima yabainishwe.

Ingawa mchezo unaweza kutafsiriwa kwa madhumuni ya kuusoma tu, mtafsiri anapaswa kulenga uigizaji jukwaani anapofanya tafsiri yoyote ya drama. Pasiwe na tofauti kati ya mchezo uliotafsiriwa kusomwa na ule uliotafsiriwa kuigizwa.

Kwa sababu hizo tulizotaja hapo juu, ni muhimu kuchunguza kuona kama mtafsiri alitilia maanani hoja hizo na kuona kama kazi tafsiri ya *Mizigo* haikulenga wasomaji pekee bali pia na muhimu zaidi, hadhira. Tasnifu hii ina madhumuni ya kuhukiki mtafsiri wa *Mizigo* katika misingi tuliyotaja hapo awali.

Uhakiki wa tafsiri una umuhimu wake katika fasihi kwa jumla. Kutokana na tafsiri, fasihi nyingi zimeathirika. Tafsiri huweza na mara nyingi hutakiwa kutekeleza jukumu maalumu katika kukuza na kuinua kiwango cha fasihi ya lugha pokezi. Hivi basi ni muhimu kuhakiki tafsiri hizi. Tasnifu hii imeamua kuchangia katika uhakiki huu unaoshughulikia tamthilia ya *The Burdens* na tafsiri yake *Mizigo*.

Tafsiri zinaweza na zimeweza kuchangia katika kukua kwa fasihi changa. Vilevile tafsiri huwezesha jamii fulani kujifunza kutokana na tamaduni za watu wa mataifa mengine mafunzo

ambayo humwezesha binadamu kupiga hatua za kimaendeleo. Wasanii nao huelimika na kufaidika kwa kusoma fasihi za wasanii wenzao katika mataifa mengine kupitia kwa tafsiri. Haya yanajitokeza katika Kiswahili hasa tunapozingatia idadi ya kazi za fasihi tafsiri zinazoingia katika lugha hii kila mwaka. Ni kupitia kwa tafsiri ambapo istilahi mpya zinaweza kubuniwa kuendeleza fasihi ya Kiswahili. Wengi wa watafsiri hubuni misamiati mipya. Tunadhamiria kuchunguza ikiwa tafsiri ya *Mizigo* tunayoihakiki inaweza kufaidi au kuleta manufaa zaidi kwa wasanii wa taifa la Tanzania ambamo tafsiri imeandikiwa, kama tafsiri hiyo imebuni istilahi mpya na kama mtafsiri amebuni msamiati bora unaofaa au la.

Ni muhimu kumnukuu P. Newmark hapa anaposema,

> "Tafsiri sio kuvusha mila na tamaduni tu bali pia ukweli na juhudi za kuendeleza ukweli katika lugha pokezi"[9] (tafsiri yetu).

Ni ufahamu wa haya ambao umetufanya tuchunguze kama tafsiri tunayoishughulikia imekuwa aminifu kwa mwandishi wa makala asilia na kuzingatia sio mila na tamaduni tu bali pia ukweli.

Licha ya udhaifu wa tafsiri, wanafasihi wengi wanaozungumza juu ya tafsiri wanadai kwamba fasihi haina budi kukopa maneno hasa kupitia tafsiri iwapo fasihi hiyo inatarajia kupiga hatua yoyote kimaendeleo. Ingawa hatupingi wazo hili, ni muhimu pia kukopa yale maneno yanayowasilisha ujumbe, yanayokubalika na kueleweka katika taratibu za lugha pokezi na utamaduni wake. Lengo la tasnifu hii ni kuchunguza na kurekebisha makosa kama hayo kwani tafsiri yoyote inaboreka kadri inapozidi kupitiwa na kukosolewa.

Kiswahili ni lugha inayokua kwa haraka sana. Njia moja ya ukuaji huo ni kupitia kwa tafsiri. Kazi nyingi kutoka lugha nyingine za ulimwengu zimetafsiriwa kwa Kiswahili. Idadi ya kazi

hizo inazidi kuongezeka ingawa dosari za tafsiri hizo hazitoweki. Ni muhimu kuonyesha na kutoa mbinu za kuchuja kazi hizo ili kuzuia dosari hizi kuingia na kuathiri ukuaji wa fasihi ya Kiswahili kwa njia mbaya[10].

P. Newmark (1988) anasema,

"Uhakiki wa tafsiri ni muhimu katika kuendeleza tafsiri yenyewe"[11] (tafsiri yetu)

Sababu moja kuu ya kuchagua somo letu ni kuhakiki tafsiri ya *Mizigo* ili kuikosoa hivi basi kuchangia katika kuendeleza tafsiri bora. Tumechagua tamthilia ya *The Burdens* kwa sababu imeandikwa katika mazingara tofauti na tafsiri yake *Mizigo*. Tunaelewa kwamba tofauti kimazingara huchangia katika kutofaulu kwa tafsiri na tasnifu hii itaonyesha athari hizo.

Ingawa mengi yamezungumziwa kuhusu tafsiri, tamthilia ni utanzu ambao haujazungumziwa sana katika dhana hii. Ni matumaini yetu kuwa huu utakuwa ni mchango muhimu katika tafsiri ya tamthilia. Yote haya kwa pamoja ndiyo yamesababisha haja ya kufanya utafiti huu.

## 1:5 HAIPOTHESIA:

1. Katika tamthilia ya *The Burdens* na tafsiri yake *Mizigo* kuna kudhoofika kwa sanaa na matumizi ya lugha kwa jumla.

2. Kuathirika kwa fani katika makala tafsiri ya *Mizigo* kumesababisha kuathirika kwa maudhui kwa jumla.

## 1:6 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI:

Kuna kazi nyingi ambazo zimewahi kuandikwa juu ya somo hili. Nyingine zimejadili swala hili

katika kiwango cha kinadharia, nyingine zimejishughulisha na utaratibu wa kutafsiri huku zikizungumza juu ya matatizo ya kijumla ya tafsiri katika kiwango cha kinadharia na kutumia mifano ya hapa ha pale kama vielelezo. Chache zimejishughulisha na matatizo ya fasihi tafsiri; chache zaidi zimejishughulisha na utanzu wa tamthilia. Utanzu wa ushairi umehakikiwa zaidi.

Mengi ya yaliyoandikwa kuhusu somo hili ni katika kiwango cha kinadharia yakizingatia dhana ya tafsiri katika mapana yake kwa kutumia makala ya lugha za kigeni kama vielelezo. Kuna pia yale yaliyoandikwa kuhusu somo hili yanayohusiana na lugha ya Kiswahili.

E. Nida. (1964; 1966; 1969) wamewahi kutoa mchango mkubwa kuhusu tafsiri. Ingawa kazi zao zimejikita katika tafsiri za Biblia, zina mengi ya kujifunza kwa kuwa zimeangalia karibu kila namna ya matatizo na taratibu za kutafsiri. Wamejadili umuhimu wa sarufi, msamiati na muundo wa lugha za tafsiri katika kiwango cha kinadharia. Kazi zao zimedhihirisha kwa kiwango fulani jinsi ya kukabiliana na matatizo halisi ya tafsiri. Kwa mapana na marefu, Nida wamejadili juu ya umuhimu uliopo katika mahusiano ya maneno, matatizo ya kutafsiri kati ya tamaduni tofauti pamoja na matatizo ya Kisaikolojia yaletwayo na tafsiri. Nida walizungumzia juu ya matatizo ya tafsiri wakijishughulisha na Biblia, tofauti nasi tunaoshughulikia sanaa katika tafsiri ya tamthilia. Hata hivyo, nadharia walizotumia na walizopendekeza zitatufaa sana katika kazi yetu.

Beekman na Callow (1974) wana mwelekeo wa kinahau katika kutafsiri, mwelekeo ambao unasisitiza mawasiliano kwa hali pana. Kuzingatia kwa mambo kama vile utamaduni, matumizi ya lugha kitamathali, muundo wa lugha, muktadha wa matumizi ya lugha, ni baadhi ya mambo wanayosisitiza. Wao wamejikita katika maandishi na tafsiri ya Biblia; tofauti na

tasnifu yetu ambayo inachuguza maandishi ya kifasihi. Mwelekeo wao katika kutafsiri utatusaidia sana katika kazi yetu.

R. A. Brower (1966) wamezungumzia umuhimu wa Tafsiri wakizingatia nafasi ya mtafsiri kulingana na madhumuni yake katika kuifanya hiyo tafsiri. Wametoa mkhutasari wa hoja kadha kuhusu kitendo na dhana ya kutafsiri. Wao wamezingatia hasa nafasi ya mtafsiri, tofauti nasi ambao tutashughulikia tafsiri ya drama. Kazi yao hata hivyo itatusaidia kwani tunanuia kuipanua kwa kuchambua makala tafsiri maalumu ya kifasihi kwa kuchunguza athari za tafsiri kwa sanaa.

J. C. Catford (1965), T. Hermans(1985), L.G. Kelly (1979), R. Kirk (1986) na M. L. Larson (1984) wote wanaelekea kusisitiza umuhimu wa mawasiliano katika tafsiri. Kila mmoja kwa njia yake anaonyesha umuhimu wa kazi ya mtafsiri kwa mujibu wa uteuzi wake ili kuwasiliana na hadhira pokezi. Wao wamezungumzia juu ya tafsiri kwa jumla tofauti nasi ambao tunashughulikia tafsiri ya tamthilia. Kazi zao zitatusaidia sana hasa kwa upande wa mtafsiri kuwasiliana na hadhira pokezi. Kazi hizi pia zitachangia katika uchambuzi utakaofanywa katika utafiti huu.

P. Newmark (1988) wanasema kwamba kuna umuhimu wa misingi ya kinadharia katika kazi yoyote ya kutafsiri. Wameorodhesha mbinu zinazochangia ujumla wa tafsiri na aina za tafsiri zinazohusika katika kutafsiri maandishi ya sajili mbalimbali katika mikitadha tofauti. Kuhusu tafsiri za drama, wamesisitiza umuhimu wa hadhira pokezi kwa mtafsiri. Ingawa wao wanasisitiza sana kuhusu misingi ya kinadharia, sisi tunashughulikia kufaulu au kutofaulu kwa tafsiri yenyewe. Kazi yao itachangia uundaji wa misingi imara ya kinadharia ambamo kazi hii

itafanyiwa.

A. Wanza (1981) wamejadili kwa mapana na marefu makosa yanayojitokeza katika taarifa za habari za sauti ya Kenya wakieleza jinsi mawasiliano yanavyopotoka katika tafsiri mbaya. Wao wametumia taarifa ya habari tofauti na sisi tutakaotumia makala ya kifasihi yaliyotafsiriwa. Kazi yao itatusaidia pale tutakapokuwa tukizungumzia juu ya kupotoshwa kwa mawasiliano.

Z. Omboga (1986) wamezungumzia juu ya fasihi tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili. Wamezingatia matatizo na athari zake hasa ubovu, udhaifu na hali ya chini ya tafsiri zinazohusika zikilinganishwa na makala asilia. Ingawa kwa pamoja tunaangalia makala ya kifasihi, kazi yetu inahusu tamthilia ilhali yao inahusu riwaya. Kazi yao itatusaidia kuangalia namna tafsiri inavyoathiri ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili.

C. W. Ryanga (1986) wameonyesha umuhimu wa kazi za tafsiri katika kukuza fasihi ya jamii fulani. Wanasema kuwa, dai kwamba vitabu vilivyotafsiriwa katika Kiswahili vina dosari hasa kwa upande wa sarufi na matumizi ya lugha ni jambo lisilokanushika. C. Ryanga wamezungumzia kuhusu tafsiri kwa jumla nasi tutajikita katika utanzu wa tamthilia. Kazi hii inaendeleza mchango wao katika kuchunguza dosari hizo katika fasihi.

N. L. Shitemi (1990) wameangalia mawasiliano katika tafsiri huku wakichunguza uteuzi wa mtafsiri na jinsi makala tafsiri yalivyoundwa kutokana na uteuzi huu. Wao wameshughulikia uteuzi wa mtafsiri nasi tunashughulikia kufaulu kwa tafsiri. Kazi yao itatusaidia kwani sote tuna mwelekeo wa kifasihi na lengo la kuchunguza mawasiliano katika tafsiri.

## 1:7 UPEO WA TASNIFU:

Tasnifu hii kwa jumla inahusu tafsiri kama inavyojitokeza katika fasihi. Ingawa tunasema kwamba tasnifu hii ni juu ya tafsiri, hatutaingilia tanzu zote za fasihi. Tutashughulikia utanzu wa tamthilia tu. Tutajikita hasa katika uchambuzi wa tamthilia iliyotafsiriwa, kwa kurejelea J. Ruganda *The Burdens* (1972) na tafsiri yake *Mizigo* (1977) iliyofanywa na Bi A. Muro.

Tutahakiki kufaulu kwa tafsiri hii huku tukichunguza na kuchambua tamthilia ya *The Burdens* na kuilinganisha na tafsiri yake *Mizigo,* tukichunguza ulinganifu na tofauti ya lugha kisanaa. Vilevile, tutalinganisha mazingara na hadhira kwa sababu makala asilia na makala pokezi iliandikwa katika mazingara tofauti, na hadhira iliyolengwa na kila makala ni tofauti pia. Aidha tutachunguza namna maudhui ya kazi tafsiri yalivyoathirika kwa sababu ya kuathirika kwa fani na lugha.

Ni muhimu kutaja hapa ya kuwa, kuna tofauti kati ya mtafsiri anayetafsiri kazi asilia isiyo yake, na yule anayetafsiri kazi ambayo mwenyewe ameiandika katika lugha asilia. J. Ruganda mwandishi wa makala asilia ameandika katika mazingara na utamaduni tofauti na Bi A. Muro aliyeitafsiri. Tasnifu hii itachunguza ikiwa tofauti katika kazi asilia na kazi pokezi zimesababishwa na hayo au la.

Baadaye tutatoa maoni yetu kutokana na uchambuzi tutakaokuwa tumefanya ili kuonyesha kiwango ambacho sanaa imeathirika na kutofautiana kati ya kazi asilia na kazi pokezi. Tutaangalia pia athari zake kwenye hatima ya tafsiri.

Tasnifu hii haitaingia katika mijadala ya nadharia ya fasihi. Pia haitaingia katika mjadala wa

kama fasihi tafsiri ni fasihi ya Kiswahili au la. Haya tutayagusia kijuujuu tu kwani kuyaingilia kutakuwa ni kukiuka upeo wa mipaka ya tasnifu hii.

## 1:8 MSINGI WA KINADHARIA:

Wakati mwingi tafsiri hutegemeana. Hakuna yoyote inayoweza kufaulu bila kutegemeana na nyingine. Kutokana na ukweli wa kauli hii, tumeamua katika tasnifu hii kutumia nadharia ya elimu-mtindo na tafsiri maana. Hii ni kwa sababu tunachunguza namna sanaa ya lugha ilivyoathirika, na kwa vile sanaa huhusu matumizi ya lugha, tutakuwa tukichunguza mtindo wa lugha. Elimu-mtindo ni taaluma ambayo hutumia maarifa ya kiisimu katika kuitalii mitindo ya lugha.

Nadharia ya elimu-mtindo pia itatuwezesha kutambua sifa muhimu zinazojitokeza katika makala asilia ya *The Burdens* na ni sifa hizi ambazo zitatumika katika kutathmini kazi tafsiri ya *Mizigo*.

Tafsiri maana nayo kwa upande wake hujaribu kuwasilisha kwa kadri inavyowezekana katika miundo ya sarufi na maana ya lugha pokezi, maana kamili ya ujumbe katika muktadha wa makala asilia[12]. Tafsiri maana hujikita katika utamaduni wa lugha ya makala na humsaidia msomaji kwa kumdokezea chembechembe za ujumbe ulioko katika makala inayotafsiriwa.

P. Newmark (1988) anasema,

> "Tafsiri maana . . . haipuuzi mambo kama vile jazanda, uteuzi kimantiki, lugha ya mitaani, lugha sanifu, simo (slang) n.k"[13].

Mwingine aliye na maoni kama ya Newmark ni C. Rabin (1958) anayesema,

> "Tafsiri ni kitendo ambamo tukio la lugha linapatikana katika lugha fulani likiwa limedhamiria kuwasilisha ile maana iliyokuwepo katika tukio la lugha lililopatikana katika lugha nyingine"[14]

Kulingana na wasomi hawa wawili, ni wazi kwamba muhimu kabisa katika tafsiri ni kuhifadhiwa kwa maana. Tafsiri maana ndiyo tafsiri halisi katika kiasi kikubwa cha tafsiri. Maoni ya wataalamu hawa yametufanya kuamua kutumia nadharia hii kama njia yetu ya mwongozo ili kuchunguza athari za kutozingatia maana katika tafsiri. Sio kwamba zile njia nyingine za tafsiri sio muhimu kwani nazo ni hatua ya kufikia tafsiri mwafaka. Tafsiri maana inastahili kuchukuliwa kama daraja mojawapo ya hatua ya mwisho na ya upeo wa juu.

Nadharia ya elimu-mtindo ambayo tutaitumia kama msingi wa nadharia imewahi kuelezewa na wataalamu tofauti kwa namna nyingi. G. N. Leech na M. H. Short (1981) wameelezea nadharia hii kuwa ndiyo inayofaa zaidi katika kutathmini mtindo wa lugha yoyote, tukichukulia mtindo wa lugha kuwa njia ambayo lugha fulani inatumika.

D. Crystal na D. Davy (1969) wanasema,

> "Matumizi ya lugha ya mtu mmoja hutofautiana na ya mwingine kama vile alama za vidole hutofautiana"[15] (tafsiri yetu).

Wamemnukuu Buffon anaposema "Mtindo ni mtu mwenyewe".

Nadharia ya elimu-mtindo huchunguza sura mbalimbali za lugha. Shabaha kuu ya nadharia hii ni kuchanganua lugha kwa nia ya kutambua sifa mbalimbali ambazo zinatumika wakati fulani, mahali fulani na ikibidi, kueleza kwa nini lugha ikatumika vile badala ya vingine [16].

Katika utangulizi wa kitabu chao *Style In Fiction* (1981), G. N. Leech na M. H. Short wamesema,

"Kuhakiki lugha katika kazi yoyote ya kifasihi kunaweza kuwa njia moja ya kuielewa zaidi na kuthamini matumizi ya sanaa ya mwandishi"[17] (tafsiri yetu).

Wanaendelea kueleza kwamba, nadharia ya elimu-mtindo huwa imefungamana kikamilivu na madhumuni ya kuelezea uhusiano kati ya lugha na matumizi ya sanaa. Hujibu maswali kama vile, kwa nini mwandishi akachagua kujieleza kwa namna hii?

Nadharia ya elimu-mtindo inafaa zaidi kwa lugha ya fasihi hata ingawa hakuna lugha isiyokuwa na mtindo. Nadharia hii pia hushughulikia maelezo ya uhusiano kati ya mtindo na matumizi halisi au sanifu wa lugha. Aidha nadharia hii huchunguza kufaulu kwa namna mwandishi fulani anavyoiendeleza sanaa yake.

Nadharia ya elimu-mtindo huwezesha kutambua ubinafsi wa mwandishi, kwa mfano, kuna waandishi ambao wana njia yao tofauti ya kueleza matukio, wana lugha ya kipekee ambayo inawatofautisha na waandishi wengine wanaotumia lugha hiyo hiyo.

Tumeamua katika tasnifu hii kutumia nadharia ya elimu-mtindo kama mwongozo wetu huku tukitumia tafsiri maana kama nadharia changizi. Nadharia hizi mbili zinawiana katika kutekeleza mahitaji ya kazi yetu. Nadharia ya elimu-mtindo itatusaidia katika kuihakiki sanaa ya makala tafsiri. Mtindo ni matumizi ya lugha inayofaa katika muktadha maalumu. Sanaa ni mojawapo ya mtindo wa mwandishi hivi basi nadharia ya elimu-mtindo itatuwezesha kutambua sifa za kisanaa katika makala asilia, sifa ambazo tutazitumia kutathmini makala pokezi. Nadharia ya tafsiri maana nayo itatuongoza katika kuchunguza kufaulu kwa kazi ya tafsiri tunayoishughulikia. Nadharia hizi mbili kwa pamoja zitauongoza utafiti huu katika kuteua misingi mwafaka itakayotekeleza yale tunayoyachunguza.

## 1:9 NJIA ZA UTAFITI:

Utafiti wetu utakuwa hasa utafiti wa maktabani. Tutasoma kazi za kinadharia kuhusu tafsiri. Tutasoma pia kazi zilizoandikwa na waliochangia somo hili la tafsiri ziwe ni tahakiki au za makala yaliyo tafsiriwa.

Tutasoma tamthilia ya *The Burdens* na tafsiri yake *Mizigo* kwa njia ya kiulinganishi ili kuweza kuangaza dosari zilizoko. Tutaangaza makosa ya kisanaa yaliyotokea na kuonyesha namna yalivyochangia katika kuipeleka kombo tafsiri hii.

Tutamhakiki Bi A. Muro kama mtafsiri ili kuweza kutambua kama makosa yaliyofanywa ni matokeo ya udhaifu wa mwandishi au yalitokana na mtafsiri kushindwa kumuelewa mwandishi wake. Kwa kuonyesha makosa hayo katika tafsiri tutakuwa tumeonyesha umuhimu wa kuhifadhiwa kwa sanaa katika kazi yoyote inayobadilika.

## Tanbihi

1. Maoni haya yametolewa na, Ombaya Z. (1986): katika tasnifu yake *Fasihi Tafsiri Katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili; Matatizo Na Athari Zake.* UK 20

2. Haya ni kwa mujibu wa, Ryanga C. W. (1985): katika *Vitabu vya Kutafsiriwa Na Fasihi Ya Kiswahili* UK 162

3. Kama hapo 2 juu UK 163

4. Haya ni maoni ya, Newmark P. (1988): katika kitabu chake; *A Text Book of Translation* UK 6

5. Maoni haya yametolewa na, Brower R. A. ed (1966): katika kitabu chake *On Translation* UK 5

6. Ruganda J. (1972): *The Burdens* UK37

7. Haya ni maoni yake, Shitemi N. L. (1990): katika tasnifu yake *Mawasiliano Katika Tafsiri: Uteuzi wa mtafsiri* UK 15

8. Kama hapo 4 juu UK 172

9. Kama hapo 4 juu UK 7

10. Kama hapo 7 juu UK 36

11. Kama hapo 4 juu UK 185

12. Kama hapo 4 juu UK 39

13. Kama hapo 4 juu UK 6

14. Haya ni maoni yake, Rabin (1958): katika kitabu chake *Aspects Of Translation* UK 123

15. Maoni haya yametolewa na, D. Crystal na D. Davy (1969) katika kitabu chao *Investigating English Style* UK 8

16. Kama hapo 15 juu UK 13

17. Haya ni maoni ya, G. N. Leech na M. H. Short (1981) katika kitabu chao *Style In Fiction* UK 9

## SURA YA PILI

### 2:1 UTANGULIZI:

Katika sura hii ya pili, tutaujadili uhusiano wa lugha ya kisanaa na uandishi wa fasihi. Tutajadili mambo kadha wa kadha ili kuonyesha namna ubora wa fasihi fulani unavyotegemea sanaa yake. Tumesema hapo awali kwamba hakuna lugha ambayo haina mtindo; hata hivyo, mtindo hutofautiana na maoni ya watu kuhusu mtindo pia hutofautiana. Maoni yetu ni kwamba, fasihi bora haina budi kuwa na sanaa ya hali ya juu. Sanaa ya mwandishi ni jinsi anavyotumia maneno ili kuitia lugha yake nakshi. Msanii hutumia maneno kwa kuvutia wasomaji. D. Lodge anasema,

> "Chombo anachotumia mwandishi kuwafikia wasomaji wake ni lugha"[1] (tafsiri yetu).

Ni dhahiri kwamba bila chombo hicho cha mawasiliano mwandishi hawezi kuwafikia wala kuwavutia wasomaji wake. Tasnifu hii inaonelea kwamba lugha ya fasihi ni sharti iwe ya kisanaa la sivyo kazi hiyo haifai kuitwa fasihi.

Katika sura hii tutajadili pia matatizo yanayokumba tafsiri na jinsi yanavyoathiri sanaa katika tafsiri. Matatizo haya ni kama vile maana, mawasiliano, nadharia na tamaduni za jamii tofauti tofauti. Yote yanaathiri tafsiri ya sanaa kwa njia tofauti. Kila moja kwa namna yake inatatiza kufikishwa kwa lugha ya kisanaa katika makala pokezi.

### 2:2 DHANA YA TAFSIRI

Kila mara, tafsiri hujaribu kuepuka matatizo ya namna mbali mbali yanayoweza kutatiza maana na mawasiliano. Matatizo ya kimaana yanahitaji kuangaliwa kwa makini sana katika muktadha wa matumizi na wa kitamaduni; kwani sababu moja kuu ya kupotea kwa maana katika tafsiri

ni tatizo la kitamaduni. Tunapotafsiri huwa tunakutanisha tamaduni mbili tofauti na huwa ni vigumu kupata visawe vya maana kati ya tamaduni zinazohusika. Ni sharti mtafsiri awe na lugha mwafaka iliyo na maana kamili ili aweze kuibuka na tafsiri iliyo na lugha inayokubalika. P. Newmark asisitiza haya anaposema,

> "...tafsiri ni ustadi ambao huhitaji lugha mwafaka na matumizi yanayokubalika. ...ni sanaa ambayo inabainisha uandishi mzuri...."[2] (Tafsiri yetu).

Mtafsiri wa kazi yoyote huhitaji kumfahamu msomaji wake pamoja na mazingira yake. Z. Omboga anasema,

> "Mtafsiri huhitaji pia kufahamu kiwango cha elimu cha msomaji huyo, umri na tabaka lake. Fauka ya hayo, mtafsiri huhitaji kujua ikiwa msomaji wake ni mtaalamu au mwanagenzi juu ya mambo yanayozungumziwa"[3].

Mwingine aliye na maoni kuhusu tafsiri ni Jacobson. Kwake yeye, tafsiri ni kama mchezo ambao huhitaji mchezaji anayeweza kuchagua na kuteua baadhi ya maneno kutoka kwa mengi aliyo nayo. Kwa mfano, katika Kiingereza kuna "he" na "she" yanayo tofautisha jinsia. Katika Kiswahili herufi "a" inatumika kuashiria iwe anayezungumziwa ni mwanamke au mwanamume. Kwa hivyo, ikiwa hakuna majina yaliyotajwa, huenda msomaji wa tafsiri asielewe kama anayezungumziwa ni mwanamume au mwanamke. Lugha ya Kiingereza inaweza kuwa na majina kama vile "boy, fellow, chap, youngster, lad, guy, lark" n.k. Yote haya yanaashiria kijana mwanamume. Huenda ikawa tafsiri ya "lark" kuwa mvulana au kijana haitakuwa na ule uzito jina hilo lililokuwa nao katika makala asilia. Haya ndiyo Jacobson anayomaanisha anaposema kwamba anayetafsiri huwa na tatizo la kuchagua neno au jina mwafaka. Ingawa mara nyingi uchaguzi hutegemea muktadha, kuna lugha ambazo hazina msamiati mwingi itakapobidi kuwe na uchaguzi wa kuteua misamiati inayofaa.

Nida na Taber (1968: 1) wanasema kwamba tafsiri si sayansi, ni ustadi, na mara nyingi kufaulu kwa tafsiri ni kipawa cha msanii. Wanaendelea kusema kuwa, ikiwa tutakumbana au kujiuliza swali ikiwa je, tafsiri fulani ni sahihi, jibu lake ni, sahihi kwa nini? Hakuna kazi mbili za tafsiri ambazo hufanana. Ikiwa makala moja itatafsiriwa na watu zaidi ya mmoja, kila kazi tafsiri itakuwa tofauti na ile nyingine.

Katika tafsiri kamili, kila sehemu ya makala asilia huwekwa katika hali ya makala pokezi. Kila sehemu ya makala asilia hubadilika kuwa makala pokezi. Ikwa kuna sehemu au sifa zilizoachwa nje basi tafsiri hiyo huwa haijakamilika. Kwa hivyo ni lazima tafsiri ifanane na kazi asilia katika kila kiwango. Catford J.C. anasisitiza haya anaposema,

> "...katika tafsiri ya kifonolojia, fonolojia ya lugha pokezi huchukua mahali pa fonolojia ya lugha asilia"[4] (tafsiri yetu).

Kuna nyakati ambapo tafsiri haifaulu. Mara nyingine mtafsiri hukosa visawe vya msamiati wa lugha asilia katika lugha pokezi. Aidha huenda akapata maneno machache sana ambayo hayawezi kuwasilisha ujumbe uliokamilika katika makala pokezi. Huenda pia maneno mtafsiri anayopata yakaweza kuwasilisha ujumbe ulio finyu. Hali kama hii hutokea kwa sababu ya lugha mbili zinazohusika kuwa na tofauti kubwa kiisimu na kinasaba.

Katika tafsiri, ni sharti mtafsiri awe mwaminifu kwa mwandishi wake. Ni lazima pia awe mwaminifu kwa lugha pokezi na tatu, kwa msomaji wa makala pokezi[5].. Mara nyingi watafsiri huenda wakakiuka kanuni za tafsiri na kueleza zaidi ya yaliyomo katika makala asilia ili kuvutia msomaji wa makala pokezi. Mara nyingine huenda akaikosoa kazi asilia ili kumvutia mwandishi wa makala hayo. Mambo haya hayakubaliki na ndiyo sababu watafsiri huitwa wasaliti yanapotokea.

Kulingana na maoni ya Costello N. (1992:18), mtafsiri yeyote ni sharti awe mwaminifu wakati wote anapotafsiri kwa lugha pokezi. Costello anasisitiza ukweli. Ukweli huu utaweza kuzingatiwa ikiwa mtafsiri ana ujuzi wa kiisimu wa lugha mbili zinazohusika. Dhamira na mtindo wa mwandishi ni mambo yaliyo na umuhimu sana na ni lazima yahifadhiwe katika tafsiri. Haya yatawezekana ikiwa mtafsiri atakuwa mwaminifu kwa mwandishi na msomaji.

Dhana ya tafsiri na umuhimu wa maana katika tafsiri ni mambo yanayokwenda sambamba na kutiliana nguvu. Tunapozungumza juu ya tafsiri, huwa tunazungumza juu ya maana wakati huo huo. Kuielezea dhana ya tafsiri ni hatua muhimu kutuelekeza kwenye tafsiri bora.

## 2:3 UHUSIANO WA MATATIZO YA TAFSIRI NA SANAA:

### 2:3:1. TATIZO LA UKOSEFU WA NADHARIA MAALUMU

Hadi hivi sasa, hakujapatikana nadharia moja maalumu kuhusu tafsiri. Jukumu la kimsingi la nadharia ya tafsiri ni kupendekeza na kuonyesha kanuni mwafaka za kutafsiria kiasi kikubwa cha kazi za namna mbalimbali. Kutoa mfumo wa maarifa, sheria za namna fulani na vidokezo vya kutafsiria makala, kuhakiki tafsiri na katika baadhi ya nyakati kutoa mbinu za kutatulia matatizo ya tafsiri. Endapo kuna ukiushi wa namna fulani katika tafsiri, mfumo huo wa maarifa unaweza kuonyesha njia mwafaka ya kuutatua na kuuepuka.

Nadharia tulizo nazo za tafsiri zina kasoro nyingi hivi kwamba hatuwezi kuziita nadharia za kisayansi. Tunatilia nguvu maoni ya P. Newmark anaposema,

> "Kwa hakika nadharia ya tafsiri si nadharia wala sayansi bali ni mfumo wa maarifa tuliyo nayo na tunayopaswa kuwa nayo kila tunapotafsiri"[6].

Kutokuwa na nadharia maalumu katika tafsiri kumesababisha matatizo mengi katika tafsiri. Kumesababishwa kwa makala ya aina yoyote kutafsiriwa kwa njia yoyote kiholela.

Kunahitajika kuwa na nadharia mahsusi kwa namna mbalimbali za tafsiri kwani ni wazi kwamba makala za aina tofauti haziwezi kutafsiriwa kwa kutumia nadharia moja. Kunahitajika kuwa na nadharia zinazotosheleza aina zote za makala.

Baadhi ya maarifa ambayo nadharia ya tafsiri ingetuwezesha kuwa nayo ni kufahamu makala inayotafsiriwa itafsiriwe vipi. Kwa mfano, lugha kitamathali, lugha ya kimzaha, lugha ya mitaani, lugha ya kuamrisha n.k. yote yawe na njia mahsusi ya kuzitafsiri. Kuwepo kwa njia kama hizi, itakachohitajika kufanya mtafsiri ni kuielewa makala anayoitafsiri, aichambue, aihakiki na atakuwa katika nafasi nzuri ya kuteua njia inayofaa ya kutafsiria kazi anayoishughulikia. Njia kama hizi pia zitamsaidia mtafsiri kwa kumdokezea ni mambo gani yazingatiwe katika tafsiri hiyo. Baadhi ya mambo hayo ni dhamira ya makala. Dhamira ya mtafsiri ni muhimu kama ilivyo ya mwandishi.

Kutokuwa na nadharia mahsusi ya tafsiri kumesababisha kudhoofika kwa sanaa ya kazi nyingi tafsiri. Mtafsiri huwa hana mwongozo maalumu na mara nyingi hutunga misamiati na dhana zake anapotafsiri, jambo ambalo huleta ukiushi katika tafsiri nyingi. Kazi nyingi tafsiri huwa zimepoteza lugha ya kisanaa inayopatikana katika kazi asilia na kupoteza ladha na uzito kitamathali. Sababu moja kuu ya kupotoka kisanaa kwa kazi tafsiri ni kutokuwa na nadharia mahsusi kwa kila aina ya makala. Lugha tofauti hutumika kwa makala tofauti na ni sharti kuwe na nadharia tofauti za kutafsiri kazi hizi.

Nadharia tulizo nazo humlazimisha mtafsiri kuelemea upande mmoja, ama wa mwandishi au wa hadhira pokezi. Z. Omboga anapinga mtindo huu anaposema,

> "...endapo nadharia ya tafsiri itaelemea upande mmoja itakuwa vigumu

kuonyesha undani na uhusiano uliopo kati ya fikra, maana na lugha"[7].

Mwelemeo kama huo hauwezi kuwa na sifa za kisayansi, iwapo tunatarajia kukabiliana na matatizo ya tafsiri katika misingi ya kisayansi. Mwelemeo huo pia hauwezi kuwa na ule mfumo wa maarifa anaoupendekeza Newmark. Tunakubaliana kwamba nadharia zilizopo zina hitilafu na dosari za kila namna ambazo zimesababisha kutofaulu kwa tafsiri nyingi.

## 2:4 SANAA NA UMBUJI KATIKA TAFSIRI

Tunapozungumza kuhusu sanaa, tunamaanisha sanaa katika mapana yake. Kutafsiri kazi yoyote ile iwe ya kifasihi, kisheria au magazeti ni sanaa, yaani kile kitendo cha kutafsiri chenyewe ni sanaa. Tunachokusudia kusema hapa ni kwamba, ikiwa kazi ya tafsiri itafanywa kwa njia isiyo ya kuisanii basi kazi hiyo haitakuwa tafsiri iliyokamilika. Kufaulu kwa tafsiri hutegemea mambo mengi ukiwemo usanii wa mtafsiri. Sanaa ya fasihi huwa katika lugha yake. Ryanga C.W. (1985:168-169) ansema,

> "Kama vile ambavyo tungo asilia zisifiwazo kwenye fasihi hutegemea uzuri na ufasaha wa matumizi ya lugha, pamoja na mbinu za kisanaa... vile vile tafsiri kama kazi nyingine za kisanaa unatokana na utamu wa mdundo wa lugha iliyotumiwa, mfululizo wa taswira na jazanda zikubalikazo katika lugha pokezi, mtiririko wa kadhia na uhifadhi wa ujumbe. Mfasiri (ibid) mweledi lazima awe na lugha yenye mdundo."

Tafsiri nyingi za Kiswahili zina dosari zinazojitokeza katika sehemu za uthabiti kama vile kuhifadhiwa kikamilifu kwa ujumbe asilia kwenye tafsiri na kwenye upande wa ufasha wa lugha. Tukitaja tu, dhamira yetu kuu katika tasnifu hii ni kuchunguza kiasi ambacho sanaa imehifadhiwa katika makala tafsiri.

*Kamusi Sanifu ya Kiswahili* (1981) inaeleza sanaa kuwa ni ufundi wa kuwasilisha mawazo yaliyomo katika fikra za binadamu ili yadhihirishe sura mbalimbali kama vile maandishi. Ni

ustadi katika chochote msanii anachofanya kiwe ni uandishi, kuchonga sanamu au kupiga muziki. Sanaa itakayotushughulisha sisi ni sanaa ya uandishi. Uandishi wa fasihi huhitaji ustadi mwingi, ufasaha wa hali ya juu na ndiyo sababu somo lenyewe likaitwa fasihi.

> "Fasihi ni bunifu, ni sanaa. Tafsiri ya toka kazi moja ya sanaa hadi nyingine huwa ya kiwango cha chini... kati ya ushairi, drama na riwaya ubora wa kazi yoyote hutegemea misingi ya sanaa na matumizi ya umbuji[8].
> (tafsiri yetu)

Tanzu wanazozungumzia wataalamu hawa ni kazi za kifasihi na maoni yao yanatilia nguvu kauli yetu kwamba uandishi wa fasihi huhitaji ustadi na ufasaha mwingi.

Katika kujadili sanaa, tumeamua kuoanisha dhana hii na ile ya umbuji kwani yote mawili yanawiana. Yote hushughulika katika kuboresha kazi yoyote ya kifasihi. Lugha kiumbuji ina malengo ya kunasa hisia za msomaji. Haya hutimizwa kwa kuzingatia sauti na ndumo zinazotumika kwa mujibu wa matumizi ya mdundo. Kwa jumla huhusu utamu wa lugha inayotumika. Sanaa nayo vile vile.

Katika uwanja wa uandishi,chombo anachotumia mwandishi ni lugha. Lugha hii ndiyo anayotumia kuijenga au kuibomoa kazi yake. Lugha ndiyo malighafi ya fasihi kama vile jiwe lilivyo malighafi ya shaba na sanamu, na rangi ilivyo malighafi kwa picha au sauti kwa muziki. Vyombo hivyo ndivyo wasanii hutumia kuunda kazi zao tofauti kisanaa. Hisia ambazo mtu huwa nazo anapoona sanamu nzuri au kusikia wimbo mzuri ndizo hizo hizo anaposoma kazi ambayo inapendeza. Hii ni kwa sababu zote ni kazi za kisanaa na sanaa ni sharti ipendeze.

Sanaa na umbuji huhusu utumiaji wa lugha ya madaha na ufasaha ili kuirembesha kazi fulani. Haya ni pamoja na kuzingatia utamu wa sauti fulani katika lugha (euphony); wiano wa

sentensi, matumizi ya jazanda, ndumo, ubadilishi wa matumizi ya kawaida ya maneno, maumbo ya kitanakali, n. k.

> "Lugha ni dirisha angavu (transparent) ambayo kupitia kwayo msomaji hutazama maisha yake. Jukumu la mwandishi ni kuiweka safi dirisha hiyo[9].
> (Tafsiri yetu)

Kusisitiza kauli hii ya Lodge D. (1966) ni lazima mwandishi aistawishe lugha yake kila anapoandika kazi fulani. Kuistawisha kazi hii ni sharti awe msanii. Kazi yoyote ya fasihi inaangazia juu ya maisha ya watu wa jamii fulani. Kama mwandishi hawezi kuangazia maisha ya jamii fulani, basi kazi zake zitakuwa mithili ya "dirisha ambalo si safi na msomaji hataweza kuona chochote."

Wasomaji wengi wa kazi za fasihi huvutiwa na sanaa ya mwandishi. Kama kazi yoyote haikuandikwa kwa ustadi, usanii na ufasaha wowote, basi kazi hiyo si fasihi na haina umuhimu kwa msomaji wa fasihi. Msanii kwa upande wa fasihi ni yule aliye na uwezo wa kuichezea lugha. Mwandishi fulani anaweza kuandika kazi kwa kutumia maneno fulani lakini kazi yake iwe inachosha. Mwingine anaweza kuandika akitumia maneno hayo hayo kwa ustadi mkubwa na kazi yake ikavutia. Kama tulivyosema hapo awali, mtindo ni mtu mwenyewe. Isitoshe, wasomaji pia hutofautiana katika maoni yao. Wengine husema kutokuwa na huo mtindo ni mtindo pia. Msimamo wetu ni kwamba, inategemea anachotarajia msomaji mwenyewe. Kwa wale wanaosoma kwa madhumuni ya fasihi, tunakariri kwamba sanaa ina umuhimu katika fasihi.

Sanders C. R. (1957) anafananisha lugha na wanawake. Anasema,

> "Maneno ni kama wanawake; hayana matokeo bora ukiyatumilia ukali; tofauti na yanapochezewa nakubembelezwa bila kubaguliwa"[10].
> (Tafsiri yetu)

Mtindo wa aina fulani ni hali ya kipekee na hakuna msanii anayeweza kudaiwa kwamba anaandika kama mwingine. Kila mwandishi anao mtindo wa kuwasilisha sanaa yake. Mtindo ukiwekwa mahali pake, yote mengine hufuatia bila tatizo lolote. Sanaa ni kama muujiza na muujiza hauji bila imani na kufanyiwa kazi, ni lazima utafutwe. Sanaa huhitaji ubunifu na msanii anabidiwa kuwa na uwezo wa kubuni na kuunda mawazo na vitu kiumbuji.

Kunao wasomi ambao hufikiria kuwa somo la fasihi ni somo la upuuzi lisilo na umuhimu wowote. Ingawa fasihi hutungwa na kuandikwa ili isomwe na kutahiniwa, jukumu lake kuu ni kufurahisha na kuburudisha. Msomaji wa makala yoyote ya kifasihi antarajia kuhisi ameburudika. Utanzu wa drama kwa mfano ni sanaa ya jamii. Fasihi yoyote inahitajika kupambwa kwa lugha ya kuvutia. Lugha ya fasihi pia huhitaji kuwa na ucheshi ili kuvunja ule mfululizo wa matukio. Lugha ya ucheshi humtegemea msanii mwenyewe, jinsi alivyo na ustadi wa kubuni na kuunda masihara.

Matatizo mengi sana hutokea wakati kazi ya kisanaa inapotafsiriwa. Masihara na ndumo yatatafsiriwa vipi? Usemi ambao mwandishi ameutumia kama sifa ya umbuji utatafsiriwa vipi? Kukosa visawe vya sifa hizi katika lugha pokezi ndiko husababisha sanaa ya lugha asilia isivuke hadi lugha pokezi. Hii ndiyo sababu kazi nyingi za tafsiri hazina ile ladha na mnato zikilinganishwa na kazi asilia.

## 2:5 MATATIZO YA KIISIMU

Kila lugha ina upekee katika vipengele vyake vya kiisimu. Mofolojia, fonolojia, sintaksia, semantiki ya kila lugha ni tofauti. Hakuna lugha mbili ambazo zina muundo wa aina moja kiisimu. Kufikia sasa, hakuna nadharia moja ambayo inazingatia miundo ya kiisimu ya lugha ya

kazi inayotafsiriwa. Hakuna nadharia inayozingatia miundo ya ndani wakati tafsiri inapofanywa.

Newmark P. (1990) katika *The Cause of Dogma in Translation Studies* amenukuliwa akisema,

> "...matatizo yanayohusiana na tafsiri yatakwisha pale muumano kiisimu na muumano kimantiki utawasilishwa katika nadharia za tafsiri"[11].
> (Tafsiri yetu)

Kutokuwa na nadharia mahususi inayozingatia miundo na mambo mengine yanayohusiana na isimu ya lugha inayotafsiriwa kumesababisha ukiushi wa mambo mengi ya lugha ikiwemo sanaa. Kutoelewa kwa miundo ya ndani ya lugha au semantiki ya lugha kunaweza kupotosha tafsiri kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, ikiwa tunatafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, tukikumbana na neno kama "contract" ni lazima tuelewe miundo yote ya neno hilo kulingana na muktadha wa matumizi yake. Ni lazima pia tuelewe maana zote za neno hilo tusije tukapotosha maana kwani neno hilo linatamkwa kwa njia tofauti ikitegemea muktadha wa matumizi. Huenda mtafsiri akaitafsiri kuwa ni kupunguza ilhali neno hilo limetumika kumaanisha maafikiano. Hapo moja kwa moja mtafsiri atakuwa ameipotosha kazi tafsiri. Maneno yaliyo na zaidi ya maana moja hukanganya wakati yanapotafsiriwa.

Watafsiri wengi wanapokumbana na matatizo ya kiisimu, hujaribu kuyaepuka kwa kutumia aina ya tafsiri ya moja kwa moja kutafsiria makala yao. Aina hii ya tafsiri huelemea upande wa lugha asilia kisarufi na kimuundo. Huilazimisha lugha pokezi kupokea maana mpya isiyokuwapo katika isimu yake. Kwa vile kila lugha ni tofauti kimuundo wa sarufi yake, miundo hii hugongana iwapo tafsiri ya neno kwa neno itatumika. Kwa bahati mbaya, hakuna nadharia inayozingatia matatizo yote ya kiisimu iwapo mtafsiri atakumbana nayo. Hii inaweza

kuwa njia ya pekee ya mtafsiri kujikwamua katika tatizo hilo.

Usahihi na uhalisi wa tafsiri inayojitokeza huathiri sarufi na miundo ya lugha ya makala pokezi. Kwa mfano, ikiwa tunatafsiri neno kwa neno methali ya Kiingereza,

> 'Not all that glitters is gold' itakuwa,
>
> Si chote king'aacho ni dhahabu.

Katika matumizi ya kawaida, methali hii husemwa kuwa chochote king'aacho si dhahabu. Mfano huu umeleta maana katika lugha tafsiri ingawa ni tafsiri ya neno kwa neno. Hata hivyo si methali na misemo yote inayoweza kuwa na maana ikitafsiriwa kwa njia ya neno kwa neno. Kwa mfano,

> "Thursday dream, Friday told, will come true, however long it takes"
>
> Alhamisi ndoto, Ijumaa isemwe, itakuja kuwa kweli, walakini urefu itachukua.

Methali ni baadhi ya matokeo ya mazungumzo ya watu wa jamii fulani. Mifano na ukweli wa kauli ya methali fulani pamoja na muktadha hupatana tu katika lugha ya jamii hiyo. Hii ni kwa sababu methali hutokana na tajriba ya wanaohusika. Methali zikitafsiriwa ni chache sana zinazoweza kuwa na maana katika lugha pokezi kwani tajriba za jamii zinazohusika ni tofauti kama vile imani zao. Tafsiri ya moja kwa moja haitaleta maana yoyote licha ya kupoteza sanaa ya lugha asilia. Fauka ya hayo, tafsiri ya moja kwa moja hazina umuhimu wa kuwasilisha ujumbe katika tafsiri kwa jumla. Larson M. L. anazipinga tafsiri za moja kwa moja akisema,

> "Tafsiri za moja kwa moja ni upuuzi na hazina umuhimu wowote katika kuwasilisha ujumbe."[12]

## 2:6 TATIZO LA KIMAWASILIANO:

Mawasiliano ni upashanaji wa habari kwa kutumia msimbo unaofahamika pande zote mbili. Haya ni kwa mujibu wa *Kamusi Ya Isimu* (1990). Kabla ya tafsiri, pande zote mbili, yaani upande wa lugha asilia na lugha pokezi huwa hauna uhusiano wowote. Ni jukumu la mtafsiri kuuvukisha ujumbe toka makala asilia hadi makala pokezi.

Ili kuelewa na kuweza kutafsiri makala asilia, mtafsiri anahitajika kufahamu hali ya mawasiliano iliyomo katika hayo makala. Ni sharti amwelewe mwandishi, dhamira aliyokuwa nayo, hadhira aliyolenga mwandishi na muhimu zaidi, mtindo alioutumia. Kuweza kutimiza haya, mtafsiri huenda akafanya ukiushi wa Kisanaa. Huenda akajipa uhuru mwingi wa kueleza mambo yaliyo nje ya tafsiri ili hadhira lengwa iweze kumwelewa. Uhuru huu ambao watafsiri wengi hujipatia huathiri sanaa ya lugha kwa kiasi kikubwa sana. Uhuru huu husababisha kupotoka, kupunguza au kuzidisha katika lugha pokezi. Costello analipinga jambo hili la kuzidisha au/na kupunguza yaliyomo anapomnukuu Steiner (1975) katika *After Babel: Aspects of Language And Translation* akisema,

> "Mara nyingi watafsiri hushambulia makala aslia, wakiondoa na kuongeza mambo mengine. Huiacha makala asila imevurugwa na ule usawa kati ya makala asilia na makala pokezi unapotea."[13]
> (Tafsiri yetu)

Nyongeza hizi za mambo yasiyokuwepo katika makala asilia huzidisha sifa hizi za makala, kubadili umbo la makala kwa kuzifinya au kuondoa sifa mbalimbali za kazi asilia. Hili hutokea katika zile juhudi za mtafsiri kujieleza ili hadhira lengwa ipate kuelewa makala kwa urahisi. Kwa kufanya hivi, mtafsiri huwa hazingatii mawasiliano bali hupoteza sanaa ya makala asilia. Zaidi ya hayo, mtafsiri huibuka na tafsiri isiyokamilika kwa sababu ya kule kurahisisha, kufupisha na kueleza baadhi ya mambo. Juhudi za kujieleza huku zinaweza kutofanikiwa na

katika kubainisha kinachomaanishwa fasiri zikawa tofauti.

## 2:7 TATIZO LA KIMAANA:

Maana katika tafsiri ni jambo la upeo sana. Tafsiri inayozingatia maana ndiyo tafsiri halisi katika kiasi kikubwa cha tafsiri. Tafsiri inayotilia maana umuhimu hujitahidi kuibuka na makala tafsiri inayokaribiana sana na makala asilia. Kusisitiza umuhimu wa maana katika tafsiri E. Nida na R. C. Taber (1968) wanasema,

> "Tafsiri huhusu utoleshaji wa sifa zote za lugha asilia hadi lugha pokezi kwa ukaribiano sana, kwanza kimaana na pili kimtindo ... maana haina budi kupewa umuhimu zaidi kwa sababu ndiyo ujumbe unaowasilishwa katika lugha pokezi."[14] (Tafsiri yetu).

Kwa kweli maana na yaliyomo ni mambo mawili ambayo ni muhimu sana katika tafsiri. Ikiwa mtafsiri ataipotosha maana, basi itakuwa amepotosha hata yaliyomo. Nam Fung Chang katika jarida lake *"Semantic" or "Communicative"* anasema,

> "Maana na yaliyomo ni kama kibao cha kukalia kilicho na miguu mitatu ...unene wa miguu hiyo unaweza kutofautiana ... lakini mguu mmoja ukiondolewa, kibao chote kinaanguka."[15]
> (Tafsiri yetu)

J. C. Catford (1965) anakubaliana na maoni hayo anaposema,

> "Tafsiri ni sharti iwe na maana sawa na makala asilia ...maana ni 'mali' ya lugha."[16] (Tafsiri yetu)

Maoni ya wasomi na wataalamu wengine kama vile M. L. Larson ni kwamba hakuna kilicho muhimu zaidi ya maana katika tafsiri. Kwake yeye tafsiri ni kuhamisha maana kutoka lugha asilia hadi lugha pokezi. Utaratibu wa tafsiri ni kutafsiri hatua kwa hatua huku mtafsiri akizingatia maana. Maana ndiyo huhamishwa hadi lugha pokezi na ni lazima ihamishwe kwa udhabiti wake.

Mwandishi yeyote anapoandika kazi yake hunuia wasomaji wake waelewe maana ya kazi hiyo. Iwapo mtafsiri atakanganyika na kuwasilisha maana tofauti na ile mwandishi aliyonuia, basi atakuwa ameinyima kazi tafsiri mambo si haba. Kwa mfano neno 'with' la Kiingereza linaweza kutafsiriwa kuwa 'na' katika Kiswahili, lakini mara nyingi matumizi ya neno hili katika Kiingereza hutegemea muktadha. Kwa mfano, "Mary with child" haiwezi kutafsiriwa kuwa Mary na mtoto. Maana yake katika Kiswahili ni kwamba Mary amehimili.

Tafsiri zinazozingatia umuhimu wa maana hujitahidi kuwasilisha maana ya lugha asilia katika hali halisi kwa lugha pokezi. Fauka ya hayo, hufikisha ujumbe katika uhalisi wa muundo kisarufi na miundo ya leksia ya lugha pokezi. J. C. Catford anasema,

> "Tafsiri iliyozingatia umuhimu wa maana haisikiki kama tafsiri. Husikika kama iliandikwa kwa lugha hiyo iliyotafsiriwa....Mtafsiri mweledi atajaribu kutafsiri akizingatia umuhimu wa maana."[17] (Tafsiri yetu)

Kwa hakika hakuna tafsiri inayoweza kuwa nzuri ama sawa na makala aslia. Kulingana na D. Lodge (1966) ni vigumu kwa msomaji yeyote aliyekomaa kusoma kazi tafsiri bila kujua kwamba kazi hiyo imetafsiriwa. Hata hivyo, jitihada huhitajika ili sanaa ya mwandishi isipotezwe na kupotea au kupotoka kwa maana. Maana ndiyo kiini cha tafsiri kwa sababu inajaribu kuleta ukaribiano zaidi kati ya lugha mbili zinazohusika kimuundo na kisintaksia. Mtafsiri anayezingatia maana huwa amedhamiria kuwasilisha kwa msomaji wake maana katika makala asilia kwa kutumia sarufi na miundo ya leksia ya lugha pokezi. Ili sanaa ya mwandishi ipate kuhifadhiwa, ili kuwe na ujumbe ulio wazi katika tafsiri, ni lazima tafsiri hiyo iwe na maana na iweze kusomeka na kueleweka. Kupotosha maana ni kupotosha yaliyomo na ni kupotosha sanaa ya mwandishi. Hutokea nyakati ambapo katika jitihada za mtafsiri kuhifadhi maana katika tafsiri husababisha kudhoofika kwa sanaa. Mara nyingi tatizo hili haliwezi kuepukika na huwa si makosa ya mtafsiri bali ni tofauti kubwa ya lugha ambazo zinahusika.

## 2:8 MATATIZO YA KITAMADUNI NA KIMAZINGIRA:

Utamaduni ni hali ya maisha na jinsi yanavyojibainisha kipekee katika jamii fulani inayotumia lugha fulani ili kuwasiliana. N. L. Shitemi anasema,

> "Tafsiri za kifasihi zinaweza kutotimia au kutoeleweka kwa sababu ya tofauti za misingi ya kitamaduni na mazingira inayorejelewa."[18]

Utamaduni unahusu umilikaji wa mali ya jamii, mila, mashirika, dhana kuhusu tabia fulani n.k. Mazingira nayo ndiyo malighafi ya lugha kwani jamii huchota lugha kutoka kwa vitu vinavyoizunguka. Tamathali za lugha huteuliwa kulingana na jinsi jamii inayohusika huzifahamu. Kila jamii inafasiri maana kwa mujibu wa utamaduni wake; hadhira pokezi itauelewa ujumbe katika tafsiri kwa mujibu wa hadhira iliyolengwa ya makala asilia.

Mtafsiri anapofanya tafsiri yake, huenda akapata majina ya vyombo vya kitamaduni au vitu vinavyopatikana katika jamii ambayo makala asilia iliandikwa lakini vyombo au vitu hivyo havipatikani katika jamii pokezi. Katika hali hii, mtafsiri huenda akatafsiri vitu vilivyokaribiana tu lakini havina uhusiano wowote. Kila mwandishi huwa na sababu maalumu ya kutumia neno, chombo au dhana fulani katika kazi yake. Mtafsiri anapopotosha haya huwa ameiuwa sanaa ya mwandishi.

Kulingana na maoni ya Z. Omboga,

> "... ni kawaida kwa mwandishi wa fasihi kutumia msamiati wa kikwao (ibid) katika kusanii kazi yake."[19]

Mara nyingi misamiati, semi na methali zinazotumika huwa zimefungamana na utamaduni maalumu. Kwa vile lugha hizi huwa ni ngumu kuzitafsiri, mtafsiri hataweza kuwa na kazi ya kisanaa kama inavyojitokeza katika makala asilia.

Kwa jumla, kutokubaliana kwa tamaduni na mazingira ya jamii nyingi husababisha kupotoka na kudhoofika kwa sanaa. Hata ikiwa kuna ule ukaribiano wa maana, matokeo kisanaa huwa si sawa.

## 2:9 MATATIZO YA KIFANI:

Matumizi ya fani katika kazi yoyote ya fasihi ndiyo upambaji anaoufanya mwandishi. Uwezo wa kutumia fani ifaavyo ni kipawa cha mwandishi. Kwa mtafsiri kuweza kutafsiri kipawa cha mwandishi ni kazi ngumu. Huweza kutafsiri ujumbe lakini matumizi ya lugha na fani ni uwezo wa kipekee. Mara nyingi mtafsiri hutatizika pale lugha ya kisanaa inagongana na masharti na mbeko za utamaduni unaohusika. Ni lazima kila lugha iendelezwe kwa adhabu zake.

Mara nyingi athari zilizonuiwa katika makala asilia huenda zisitimizwe kutokana na kutofahamu misingi ambamo hayo matumizi yamejikita hasa pale ambapo fasiri mbaya ya tamathali za usemi zinahusika. Licha ya ugumu katika kutafsiri; kupata kisawe mwafaka kwa ujumbe fulani kiumbuji humtatiza mtafsiri. Hutegemea ujuzi na uwezo wake katika matumizi ya lugha asilia na lugha pokezi kijazanda.

Katika kutafsiri fani ya lugha, ni lazima mtafsiri aichuje lugha hiyo kama haikubaliani na adhabu na mbeko za jamii anayotafsiria. Ikiwa katika makala asilia mwandishi alitumia lugha butu, mtafsiri atajaribu kuukwepa ule ukali wa matusi na kujaribu kuupoza au atumie tauria ya lugha pokezi. Kufanya hivyo atakuwa moja kwa moja ameiathiri sanaa ya mwandishi na makala tafsiri yatakosa huo ufundi.

> "Si kwamba uteuzi huu ndio unafaa lakini kuufikia bila shaka mtafsiri huwa ameulinganisha na mambo mengine na kuufikia kama ndio unaofaa."[20]

N. L. Shitemi naye anasema,

> "Mara nyingi si rahisi kutafsiri athari za matumizi fulani ya lugha kiumbuji bila kuhusisha ukiushi. Ingawa ndumo na jazanda ni sifa muhimu za kiumbuji, si rahisi kutafsiri kwa sababu ya kutoelewa au kutopatikana katika utamaduni na mazingira ya lugha pokezi."[21]

Wahusika hatutawaacha nyuma tunapozungumzia kipengele hiki cha fani. Mbali na zile tabia zao, wahusika huweza kuwa na majina ya kilakabu au hata kuwa na majina yenye maana ya kimajazi kwa sababu misingi ya tamathali hizi huwa katika lugha na utamaduni wa lugha asilia, maana yake inapotea katika lugha pokezi kazi hiyo inapotafsiriwa. Fani yote kwa jumla huathirika inapotafsiriwa hadi lugha nyingine kiasi cha kuumbua sanaa ya lugha inayopatikana katika kazi tafsiri.

Sio kwamba jazanda na fani nyingine za kisanaa ziachwe nje wakati tunapotafsiri. Ni muhimu kujaribu kutafsiri vivyo hivyo kwa sababu ni sifa za ziada za kiisimu ambazo hueleza ulimwengu wa kiakili na kuuhusisha na mapito fulani ya kilimwengu. Umbuji wa mtafsiri hauwezi kutenganishwa na uteuzi wa umbo, mtindo, maana na ukiushi unaofanywa. Yote husaidiana kwa pamoja ili kutoa kisawe mwafaka cha makala asilia. good piece of work



FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

## 2:10 HITIMISHO

Katika sura hii tumeonyesha na kujadili dhana ya sanaa kama inavyojitokeza katika lugha ya mwandishi wa fasihi . Sura hii imejaribu kueleza matatizo yanavyokumbana na mtafsiri yeyote na namna matatizo hayo yanavyoathiri sanaa katika lugha pokezi.

Itakumbukwa kwamba tafsiri iliyokamilika hutegemea kipawa cha mtafsiri. Ingawa watafsiri hujitahidi kuteua visawe katika lugha pokezi, ni nadra sana kuweza kupata visawe vya lugha ya sanaa kwani kila lugha huwa na upekee katika matumizi yake ya sanaa. Ingawa mtafsiri anatakiwa kuwa mwaminifu kwa mwandishi, hutokea nyakati ambapo hukumbwa na matatizo mengi hivi ikambidi kukiuka uaminifu huo. Mwandishi na mtafsiri wote ni watu wenye ubinafsi wao na mtafsiri anaweza kuibuka na mitazano tofauti pale ambapo atatatizika na ukosefu wa visawe.

## Tanbihi

1. Lodge D. (1966): *Language of Fiction*. Routledge and Kegan Paul Plc; London. UK1

2. Newmark P. (1988): *A Text Book of Translation*. Prentice Hall International (UK) UK 6

3. Zaja O. (1986): *Fasihi Tafsiri Katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili*: Matatizo na Athari Zake. UK 32

4. Catford J. C. (1965): *A Linguistic Theory of Translation*. Oxford University Press (UK) UK 94

5. Costello N. (1992): *On Translation Theories*. Notes on Translation, Journal, Texas U.S.A. UK 19

6. Kama hapo 3 juu UK 31

7. Kama hapo 3 juu UK 35

8. Wellek R. & Warren A. (1949): *Theory of Literature*. Jonathan Cape, Great Britain, UK 21

9. Kama 1 hapo juu UK 3

10. Sanders C. R. (1957) Lytton Strachey: *His Mind And Art*. O.U.P. Yale University Press. UK 287

11. Kama 5 hapo juu UK 3

12. Larson M. L. (1984): *Meaning-Based Translation*. A Giude To Cross-Language Equivalence. University Press of America Inc. UK 15.

13. Steiner (1975): *After Babel: Aspects of Language And Translation.*

14. Nida E. & Taber R. C. (1968): *The Theory And Practice of Translation*. UK12.

15. Kama 5 hapo juu UK 35.

16. Kama 4 hapo juu UK 35.

17. Kama 4 hapo juu UK 16.

18. Shitemi N. L. (1990): *Mawasiliano Katika Tafsiri*: Uteuzi Wa Mtafsiri. Tasnifu ya M.A. U.O.N. Haijachapishwa.

19. Kama 3 hapo juu UK 71

20. Kama 3 hapo juu UK 46

21. Kama 17 hapo juu UK 60

## SURA YA TATU

### 3:1 UTANGULIZI

Swala la muhimu tutakalolishughulikia katika sura hii ni kwamba, tafsiri ya *Mizigo* katika Kiswahili ina udhaifu katika upande wa sanaa. Tunamaanisha kwamba lugha yake ni ya kiwango cha chini kiumbuji ikilingasnishwa na lugha ya makala asilia *The Burdens*. Tutazungumzia swala hili kwa kuonyesha mifano ya makosa mbalimbali yanayojitokeza humo. Tutazungumzia pia sababu zilizosababisha udhaifu huu unaojitokeza huku tukijikita katika misingi ya nadharia ya elimu-mtindo na tafsiri maana. Tutajaribu kuonyesha ni kwa kiwango kipi nadharia na taratibu za elimu-mtindo na tafsiri maana zinaweza kutumiwa kukabiliana na udhaifu kama huo.

### 3:2 UHAKIKI WA MIZIGO

Tafsiri ya *Mizigo* imefika katika Kiswahili ikiwa imenyimwa mambo mengi ya lugha kiujumi (aesthetics). Makosa haya yamejitokeza katika viwango mbalimbali. Yamejitokeza katika lugha ya kitamathali hasa katika makosa yanayotokana na tafsiri mbaya za lugha ya kitamathali na kunga nyingine za lugha na utunzi, tafsiri za moja kwa moja ambazo zinasababisha kutoeleweka kwa mtafsiri na pia kudhoofisha sanaa ya kazi hiyo, tafsiri mbaya za ushairi zinazosababisha kupotea kwa maana, mdundo na ladha ya ushairi kwa jumla na kutofaulu kusawiri kwa wahusika kama wale wanaopatikana katika makala asilia.

Kuweza kuwa katika nafasi nzuri ya kuihakiki tafsiri hii inavyopaswa, hatuna budi kubainisha mambo machache. Ili kuthibitisha udhaifu tunaozungumzia, itatubidi kuirejelea kazi ya *The Burdens* mara kwa mara. Kuirejelea kwetu kutatuwezesha kuonyesha sifa za kifasihi ambazo zimefinywa au zimeachwa nje kabisa katika tafsiri. Kufanya hivi pia tutakuwa tunaitathmini

kazi hii kama kazi ya kifasihi, yaani kazi tafsiri ikilinganishwa na kazi asilia. Ni muhimu kuisoma na kuelewa kazi yoyote ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuitafsiri. Kufanya hivyo humwezesha mtafsiri kufahamu barabara anachokitafsiri. Hukumu na kauli atakazozitoa kuhusu kufanikiwa au kushindwa kuitafsiri hutegemea umaizi wa mtafsiri wa kazi hiyo.

Ni muhimu kutaja hapa kuwa, kuirejelea kazi asilia kutatuwezesha kuifasiri vizuri kazi yenyewe na kisha kutumia ufasiri huo kama kigezo cha kupimia kufanikiwa kwa tafsiri ya *Mizigo*. Katika kufanya hivyo tutakuwa tukifuata utaratibu wa kuhakiki tafsiri ya mafungu yote tutakayoyatumia kama mifano katika kazi asilia tukizingatia hatua mbalimbali za kutafsiri kwa mujibu wa wiano uliopo kati ya lugha zinazohusika.

Kipengele cha lugha ni muhimu sana katika kazi yoyote ile ya sanaa ya kifasihi. Matumizi ya lugha ndiyo yanayofanya kazi fulani ionekane tofauti na nyingine, na ndiyo hutofautisha kazi ya sanaa ya kifasihi na ile isiyo ya kifasihi. Tutazingatia pia mambo mengine kama vile dhamira ya mwandishi, maudhui yaliyokusudiwa, matarajio ya msomaji na vile vile adabu ya lugha pokezi.

### 3:1 TAFSIRI YA LUGHA YA KISHAIRI

Ushairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo unaoeleza wazo fulani, hisi au tukio juu ya maisha na ambao hufuata utaratibu wa urari na muwala maalumu unaoheshimu na kuzingatia kanuni za utunzi wa ushairi unaohusika. Haya ni kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981). Ingawa kuna ushairi huru ambao umekubalika katika fasihi, hatutajishughulisha na aina hiyo ya ushairi. Hii ni kwa sababu kazi tunayoishughulikia imetumia ushairi uliofuata utaratibu na kanuni za utunzi

wa mashairi.

Kutafsiri lugha ya kishairi ni jambo gumu kwani kupata urari na mdundo wa shairi fulani katika lugha pokezi sio rahisi. Mwandishi wa *The Burdens* ametumia lugha ya kishairi na kuipamba lugha yake kwa maneno yaliyo na sauti moja (sing song). Hii ni moja ya fani ya kisanaa iliyoendelezwa vizuri sana katika kazi asilia na ambayo imeathirika si haba katika kazi pokezi. Mtafsiri wa *Mizigo* alijitahidi lakini aliibuka na maelezo tu badala ya ushairi. Kutojitokeza kwa ushairi huu katika kazi tafsiri kumesababisha udhaifu mkubwa kisanaa katka tamthilia nzima, na kwa kiwango fulani pia kuathiri usawiri wa wahusika. Ruganda ametumia lugha kwa ustadi mkubwa kuwasawiri wahusika wake. Ni mwandishi anayetumia wahusika kama mdomo wake, kusema anachotaka kukisema na jinsi anavyotaka kukisema. Ruganda anafanya lugha imtumikie. Moja ya sifa zake ni kutumia wahusika kuonyesha ubunifu alionao Ruganda. Ushairi huu kukosekana katika kazi tafsiri kunaonyeshana wahusika ambao si wabunifu na matokeo yake ni kwamba wahusika wa kazi asilia na wale wa kazi pokezi wanatofautiana. Mifano ifuatayo inaonyesha athari za tafsiri hizi;

Makala Asilia UK 2

Kaija: *Booklax clears the stomach*, he says.

Makala Pokezi UK 3

Kaija: Yeye husema kuwa *Brooklax inasafisha tumbo.*

Katika mfano huu, kazi asilia ina ile sifa ya kukokoteza sauti kwa sababu jina "Brooklax" inakaribiana kimatamshi na "clears" na "stomach" hasa katika silabi za mwisho. Tafsiri ya Kiswahili haijitokezi hivyo kwa sababu jina "Brooklax" ni la Kizungu na hakuna jina la Kiswahili linalokaribiana kimatamshi nalo. Kwa sababu hii, maneno yanayojitokeza katika

lugha asilia yana uzito zaidi kisanaa kuliko maneno yaliyo katika tafsiri. Hatutarajii mtafsiri kubadilisha jina la bidhaa ili kuwa na sauti zinazofanana kimatamshi. Ni sababu kama hizi za kutokuwa na visawe katika lugha pokezi ambazo zimesababisha kutoweka kwa huo urari wa sauti. Kuna mifano chungu nzima ya aina hii inayojitokeza katika tamthilia nzima;

Makala Asila UK 10

| | |
|---|---|
| Kaija: | Which others? |
| Tinka: | *Chiefs and thieves.* |
| Kaija: | *Thieves or Chiefs*? |

Makala Pokezi UK 11

| | |
|---|---|
| Kaija: | Wengine wapi? |
| Tinka: | *Machifu na wezi.* |
| Kaija: | *Wezi au Machifu*? |

Katika tafsiri hii, tunapata kwamba kule kukokoteza kwa sauti kana kwamba zinakaririwa hakupo. Hii ni kwa sababu "chiefs and thieves" ya Kizungu ni maneno yanayotamkwa karibu sawa, tofauti na "machifu na wezi" ya Kiswahili.

Katika *The Burdens*, tunapata kuwa mwandishi anatumia neno "like" kufananisha Kaija na babake. Ametumia neno hilo kwa ustadi mkubwa kama tunavyoona katika (UK 12). Tinka anasema "like father like son" maneno ambayo yametafsiriwa kuwa "ni ya mwana kufuata nyayo za babake" katika *Mizigo*. Mtafsiri ameeleza tu yaliyomaanishwa na mwandishi wala hakuhifadhi ule ufundi aliosema nao maneno haya mwandishi. Kuna mifano mingi ya fasiri badala ya tafsiri katika kazi tafsiri.

Tamthilia hutumia mazungumzo kwa wahusika kupokezana katika mazungumzo hayo. Katika

kazi asilia ya *The Burdens* wahusika wanapokezana kwa ustadi mkubwa, hali inayoleta mdundo fulani. Tuna mfano ufuatao;

Makala asilia UK 17

| | |
|---|---|
| Voice: | Thank you, thank you very much for helping me. I couldn't have managed that *bed*... |
| Kaija: | The *bed*? |
| Tinka: | To *bed* at once. |

Makala pokezi UK 19

| | |
|---|---|
| Sauti: | Ahsante sana kwa kunisaidia. Singeweza kukibeba hiki *kitanda* peke yangu... |
| Kajia: | *Kitanda*? |
| Tinka: | *Ukalale* upesi. |
| Kaija: | *Kitanda* mama. |
| Tinka: | Nenda *Kalale* upesi. |

Katika kazi asilia, neno "bed" limetajwa na kila mhusika kwa njia na maana tofauti. Huu ni mtindo wa mwandishi kurudia neno hili makusudi. Angesema "go to sleep" badala ya "to bed" ambayo yote yana maana sawa. Nia yake ilikuwa ni kuichezea lugha jambo ambalo mtafsiri hakufaulu kulifanya. Mtafsiri hakuweza kulirudia neno kitanda kama inavyojitokeza katika kazi asilia. Jambo hili limeathiri mtindo wa mwandishi licha ya kudhoofisha sanaa ya makala tafsiri.

Mfano mwingine ni pale mwandishi anakariri neno "big" kuonyesha dhihaka, bezo na dharau dhidi ya wale wanaopora mali ya umma kujitajirisha. Anasema,

Makala asilia UK 23

Wamala: I'll tell you my girl. This is luxury. The opium of the bourgeoisie. *Big* business, *big* mansions, *big bottomed* wives.

Makala pokezi UK 25

Wamala: Mke wangu, nitakwambia. Hii ni anasa tu. Ni kasumba ya kibepari. Biashara *kubwa kubwa*, nyumba *kubwa kubwa* na wanawake *wanene wanene*.

Mwandishi ametumia mfano wa watu wa mfumo wa kibepari ambao wanalimbikiza mali na ametumia lugha ambayo imetoa vizuri sana wazo hilo. Ameweza kulikariri neno "big" na kuleta taswira ya watu walio na tamaa sana. Wanataka kila kitu kwa wingi na ukubwa wake. Mtafsiri hakuitoa sehemu hii kama inavyojitokeza katika makala asilia. Tafsiri ya sehemu hii haina mnato wa kifasaha kama ule tunaopata katika makala asilia. Ni chapwa na hafifu ikilinganishwa na ile sehemu inayopatikana katika makala asilia. Mtafsiri hakuweza kuifululiza neno 'kubwa' kama mwandishi anavyofanya. Mwandishi hakukusudia kusema wanawake wanene. Alitaka kutumia lugha ya kuwabeza wake wa wale matajiri kwa kuwaita wanawake walio na matako manene (big-bottomed wives). Ingawa neno nene lina maana sawa na kubwa, mtafsiri angetumia neno kubwa mfululizo kama alivyofanya mwandishi. Isitoshe, mtafsiri anajaribu kuukwepa ukali wa matusi ya mwandishi na kujaribu kuupoza. Lugha hii ya mtafsiri inaathiri maudhui aliyokusudia mwandishi. Maudhui ya uozo wa jamii hasa tukizingatia Uganda ambayo hadi hivi majuzi imekuwa na vurugu nyingi za kisiasa.

Huenda ikawa kwamba mtafsiri amezuiliwa na adabu ya lugha pokezi kwa sababu yakitafsiriwa hivyo yataudhi. Huenda ikawa pia mtafsiri hakuyapa umuhimu wowote maandishi haya; na hili ni jambo la mjadala maanake tunaelewa kwamba adabu ya lugha

inaweza kuwa tatizo katika tafsiri. Hata hivyo, hatuwezi kumtetea mtafsiri kwasababu kulingana na mifano tutakayoitoa baadaye, anakiuka jambo hili la kuiwekea lugha pokezi adabu zake. Mtafsiri hakuzingatia maana wala elimu-mtindo katika tafsiri yake ndiposa akawa na matokeo kama haya.

Katika makala asilia (Ukarasa 28-30) tunapata lugha ya kishairi ambayo imebadilisha katika makala tafsiri.

Uk 28

"Put a tiger in your tank" "mtie chui katika tanki lako"

Tafsiri hii haileti ule mdundo wa "Tiger and Tank" katika makala tafsiri. Ambapo katika makala asilia, neno "Tiger" na neno "Tank" yanatamkwa karibu sawa, Chui na Tanki yana tofauti kubwa kimatamshi. Kuna mifano zaidi ya aina hii.

Wamala: *Waragi wins thighs*

Tinga: What?

Makala pokezi uk 29

Wamala: *Waragi huyashawishi mapaja*

Tinka: Nini?

Mwandishi ametumia neno "Waragi" ya Luganda kusudi ipate kuwa pamoja na neno "Thighs" la Kizungu. Ni kawaida ya wasanii wengi kutumia msamiati wa kitamaduni katika kuisanii kazi yao. "Waragi" ni aina ya pombe ambayo mwandishi ananuia kusema kwamba inafanya wanawake kushawishika kwa urahisi wakishainywa. Kwa kutumia msamiati wa Luganda, msanii ameweza sio tu kutumia maneno yaliyokaribiana kimatamshi bali pia kuipa kazi yake ya kifasihi utambulisho maalumu. Kufanya hivyo pia huwezesha kazi fulani kuhusishwa na utamaduni maalumu. Mtafsiri amefaulu katika kuitafsiri sehemu hii, lakini usanii ulio katika

makala asilia hauko katika makala tafsiri. Ni kwa sababu ya kutokuwa na kisawe ambacho matamshi yake yangekuwa karibu na ya mapaja. Ni jambo la busara pia kuuacha msamiati wa kitamaduni bila kuutafsiri ikiwa ukitafsiriwa utakanganya.

Mfano mwingine wa tafisiri inayokosa mdundo kama katika makala asilia tunaupata katika makala asilia uk 28.

Wamala: DRINK VAT FOR VIRILITY

Makala pokezi uk 30.

Wamala: KUNYWA VAT UWE MWANAMUME.

Tafsiri hii kwa sababu ya kukosa kisawe cha jina la bidhaa "VAT" imeathiri sio sanaa peke yake, bali pia kutoeleweka kwa mtafsiri. Haieleweki kinagaubaga sababu iliyomfanya mtafsiri kulitafsiri neno "VIRILITY" kuwa mwanamume. "Virility" ni nguvu za kiutendaje katika kufanya mapenzi. Mtafsiri alitaka kuandika kwa kifupi kama mwandishi hivi basi akatoa tafsiri mbaya. Fauka ya hayo, mtafsiri hakuzingatia maana ya muktadha. Nguvu za kiutendaji katika kufanya mapenzi hazina wanaume peke yao, bali pia wanawake. Akili na mawazo ya mhusika Wamala yameongozwa na hali ya maisha anayoishi, na hali ya jamii anamoishi. Jamii yote imeoza na mawazo yao yote yamo katika mambo machafu machafu. Haya ni baadhi ya maudhui aliyo kusudia mwandishi. Kutokana na mfano wa tafsiri ya sehemu hiyo na sehemu nyingine tutakazohakiki baadaye, maudhui haya yamefinyika katika kazi tafsiri.

Kuna mifano zaidi kama hii,

Makala Asilia uk 28.

Wamala: REX AND SEX FOR A MAN OF TASTE

Tinka: You're dirty minded.

Wamala: The only thing that works these days.

Tinka: Dirt?

Wamala: *Sex* . Our new religion, forgeting alcohol for a moment.

Makala pokezi uk 31

Wamala: REX NA NGONO KWA MWANAMUME MWENYE MATAMANIO

Tinka: Una mawazo machafu.

Wamala: Hayo ndiyo mawazo yanayofanya kazi siku hizi.

Tinka: Uchafu?

Wamala: *Wanawake.* Ndiyo dini yetu mpya tukiweka pombe pembeni kwa muda.

Huu ni mfano mwingine wa tafsiri ambayo haikuzingatia sanaa ya mwandishi ya takriri. Sababu hii basi imesababisha kuvunjwa kwa mfululizo huo. "REX" ni aina ya sigara na mwandishi aliiweka neno hilo hapo kusudi liambatane na "Sex" na "Taste" ili kuleta ule urari wa lugha ya kishairi. Kwa sababu ya kutofautiana kwa miundo ya lugha, sanaa ilidhoofika na tafsiri hiyo kupotoka. Neno 'Ngono' anayotumia mtafsiri ina matokeo ambayo yana athari kubwa katika lugha ya kiswahili, neno ngono halina uhusiano kimatamshi na 'Sex'. Ingekuwa bora kama mtafsiri angetumia neno mapenzi badala ya ngono.

Tumesema hapo awali kwamba huenda mtafsiri anachelea miiko ya lugha ya kiswahili na ndiyo sababu hakulitafsiri neno matako. Viwango vya mwiko vya neno 'matako' na neno 'ngono' havilingani na kama ilikuwa vigumu kwa mtafsiri kulitafsiri neno matako, imekuwaje ataitafsiri neno ngono. Baadaye katika sehemu hii anaitafsiri neno 'Sex' kuwa wanawake. Kwa sababu ya tafsiri hii ya 'Sex' kuwa wanawake, mtafsiri anaipotosha kazi asilia. Mazungumzo

yanayomalizia sehemu hii hayaeleweki vizuri katika kazi tafsiri kwa sababu yamefungamana na mazugumzo ya sehemu hii. Mwishoni mwa onyesho tunapata mazungumzo haya,

Makala Asilia uk 44.

Tinka: Let's go to bed

Wamala: What time is it?

Tinka: About two, I think

Wamala: I'll have another shot. And off to bed.......

Tinka: *You said it's the only thing that works*

Wamala: *the drink?*

Tinka: *No. You know..... the other thing.*

Wamala: *Oh, the only thing that works these days (he laughs hopefully)*

Tinka: *When are you around, remember?*

Makala pokezi uk 48

Tinka: Twende tukalale

Wamala: Ni saa ngapi?

Tinka: Ni kama saa nane hivi

Wamala: Nitakunywa bilauri nyingine moja halafu nikalale

Tinka: Ulisema ndicho kitu pekee kifaacho.

Wamala: Pombe?

Tinka: Hapana, unafahamu..... kile kitu kingine

Wamala: Ndicho pekee kifaacho siku hizi (anacheka kwa matumaini)

Tinka: Unapokuwa hapa, unakumbuka?

Kwa sababu ya tafsiri ya 'Sex', kuwa wanawake hapo awali, msomaji wa kazi tafsiri hataelewa

ni kitu gani kinachozungumziwa na ambacho *ndicho kitu pekee kifaacho siku hizi.* Tunaposoma kuwa Wamala anacheka kwa matumaini, si rahisi kuelewa anatumainia nini. Kwa sababu ya kuvunjwa kwa muumano huu, mtafsiri ameua ustadi wa mwandishi wa kuleta mbinu ya ucheshi kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mtafsiri hakuzingatia umuhimu wa maana aliyokusudia mwandishi, wala hakufanya tafsiri yake katika misingi ya elimu-mtindo. Ndiposa mtindo wa mwandishi ukapotea na tafsiri hiyo ikayumbayumba.

Ushairi wa mwandishi tunaupata katika maneno anayoyatumia ambayo yanaweza kukumbukwa kwa urahisi (slogans). Mwandishi, kupitia kwa mhusika Wamala, amebuni maneno yaliyo na urari wa sauti. Majina na sifa anazowapa watu hawa yanaanzia na 'V'. Si lazima kung'ang'ania urari wa sauti kama huu na ndiyo sababu hatumhukumu mtafsiri katika misingi hii. Hata hivyo, kutokuwa na urari wa sauti katika kazi tafsiri kumeathiri mtindo wa mwandishi.

Kuna mifano ufuatayo,

Makala Asilia uk 30

Wamala: (showing off) 'VOTE VIGOUR; VOTE VETERAN VINCENT......
VOTE VETERAN VINCENT?

Makala pokezi uk 33

Wamala: (kwa maringo) MCHAGUE SHUJAA; MCHAGUE VINCENT
MWENYE MAARIFA.... VINCENT, MCHAGUE VINCENT
MWENYE MAARIFA?

Mtafsiri ametafsiri yale mwandishi aliyomaanisha, lakini ule mdundo wa ushairi na matumizi yanayoweza kukumbukwa kwa urahisi hayapo katika kazi tafsiri. Mifano mingine ni,

Wamala: I said he would use the three V's dimension attack. VOTE VALOUR;

VOTE VALUE; VOTE VINCENT.

Tafsiri - Wamala: Ninakwambia kuwa kwa upande wake ungeweza kutumia maneno kama: MCHAGUE SHUJAA; MCHAGUE ANAYEFAA; MCHAGUE VINCENT.

Makala Asilia

Tinka: VOTE VAPOUR; VOTE VIOLENCE; VOTE VENGEANCE; VOTE VINCENT. You see. You forget what damage the opponent could inflict on your V's rubbish.

Makala pokezi

Tinka: CHAGUA NDOTO; CHAGUA UTUMIAJI NGUVU; CHAGUA KISASI; MCHAGUE VINCENT. Unaona. Umesahau kabisa jinsi anavyoweza kuyageuza maneno yako hayo ya kipuuzi.

Mwandishi alinuia kuwa na madondoo ya kudondoleka (Quotable Quotes) kama asemavyo yeye. Katika tafsiri, hayajitokezi hivyo kwa sababu jina Vincent linalingana kimatamshi na maneno mengine yanayo tumika katika kazi asilia. Kwa sababu ya miundo tofauti ya lugha hizi mbili, jina Vincent halingeweza kuambatana na maneno ya Kiswahili ambayo yamekaribiana kimatamshi. Matokeo yake ni kwamba sanaa ya mwandishi imedhoofika katika makala pokezi. Makosa yanayo jitokeza hapa si ya mtafsiri, bali ya lugha kutofautiana.

Katika utanzu wa tamthilia mwandishi huwa hawezi kujieleza na kwa sababu hii anatumia wahusika wake kufanya hivyo. Ameumba mhusika Wamala kama mtu aliye na akili nyingi na mwenye usemaji uliyo na ufasaha. Ana maneno yanayovutia. Bibi yake wamala ambaye ni mhusika mwingine kwa kiasi fulani naye ni hivyohivyo. Mambo na tabia muhimu kuhusu wahusika hawa wawili hayakujitokeza katika kazi tafsiri kwa sababu ya lugha waliyotumia

kuathirika katika kazi tafsiri. Tinka ambaye anaonekana kuwa mwenye kupenda vurugu katika makala asilia ni tofauti kabisa na yule aliye katika kazi pokezi. Kwa jumla, wahusika tunaowapata katika kazi asilia ni tofauti kabisa na wale walio katika kazi pokezi.

## 3:4 TAFSIRI ZA KITAMATHALI

Sababu muhimu ya matumizi ya lugha kitamathali katika kazi ya fasihi au maandishi mengine ni kueleza kwa undani na kwa ufasaha tukio au matukio kwa njia ya mkato iliyo bainifu zaidi na isiyo tumia lugha ya moja kwa moja. Lugha ya moja kwa moja huwa dhaifu ikilinganishwa na lugha kitamathali katika maandishi ya fasihi. Waandishi hutumia tamathali za usemi kuitia lugha yao nakshi na kuiboresha sanaa yao.

Katika kazi tunayoishughulikia, mwandishi ametumia sitiari, taswira, taashira, methali, misemo, tashbiha na nahau chungu nzima. Tamathali hizi zote zimetumika kwa ustadi sana na zimeeleza kwa ubainifu zaidi maudhui na dhamira. Nyingi ya tamathali hizi zina undani sana. Kuzitafsiri kwa njia isiyo zingatia maana kunaweza kuzipotosha au kusababisha kuweko kwa mambo yasiyofungamana na yaliyomo. Vilevile kunaweza kuleta maana tofauti na isiyoeleweka au kuipotosha maana yenyewe kabisa. Kuna mifano kemkem ya upotoshi wa lugha ya kitamathali katika kazi tunayoihakiki jambo ambalo limeathiri maudhui ya mwandishi na mtindo wake kwa kiwango kikubwa. Mwandishi alitambua kuwa bila umbuji wa mfumo maalumu wa kujieleza maudhui yake hayawezi kubainika ndiposa akatumia tamathali.

### 3:4:1 TAFSIRI YA METHALI.

Methali ni kazi ya sanaa ya kifasihi ambayo kwa kawaida hutumia mafumbo. Semi zote kwa jumla zina hekima ndani yake. Ubora wa hekima hiyo hutegemea muktadha wa matumizi ya methali hiyo. Methali pia ina kazi ya kufurahisha, kutisha, kuonya, n.k. Kila wakati mwandishi anapotumia methali kama sitiari hakusudii kueleza maana ya methali hiyo, anaitumia kueleza mambo fulani katika muktadha fulani maalumu. Kuitafsiri methali hiyo moja kwa moja humwingiza mtafsiri katika hatari ya kupotosha kazi asilia kimaana. Methali na tamathali nyingine kama hizo huwa zinahusiana na utamaduni fulani maalumu na hutaka zitafsiriwe kimaana.

Mwandishi anapoitumia methali hakusudii ieleweke kwa maana yake asilia moja kwa moja. Hutaka ieleweka kulingana na muktadha wa matumizi yake. Kwa sababu hii, kutafsiri methali hutaka mtafsiri azingatie sana mkutadha. Ni sharti pia afahamu kila mara kwamba methali hufungamana na utamaduni fulani. Kila mara, mtafsiri sharti ajiepushe na utumiaji wa methali za kubuni au za lugha yake ambazo huenda zikaleta maana tofauti au isiyoeleweka zikiwekwa katika muktadha wa methali inayotafsiriwa na maana kimuktadha. Ifuatayo ni mifano ya makosa yaliyofanyika katika tafsiri ya *Mizigo.*

Makala Asilia uk 6

Tinka: He has never been up, Kaija, I want you to know that. Never been really up, as high up as men like Isaza or Isimbwa. *A lamb is not a lion*, son.

Makala pokezi uk 6

Tinka: Hajawapo mtu mkubwa wa hali ya juu, Kaija, nataka ulifahamu hilo. Hajainuka na kuwa juu, kama akina Isaza au Isimbwa. Mwanangu, *mwana kondoo si Simba.*

Makala Asilia uk 8

Tinka: Let them. You won't do a thing like that. No. How can I bear the derisive laughter of the slum women? Their shocked whispers. Their malicious gossip. Their mock pity. *A maimed Tigress dies clawing at the soil son.* Don't put your mother's pride at stake.

Makal pokezi uk 9

Tinka: Acha wauze lakini wewe hutafanya kitu kama hicho. Hapana. Nitawezaji kuvumilia vicheko na dharau za wanawake wa mtaa huu wenye vibanda? Minong'ono na masengenyo yao, umbea, *chui jike aliye kilema hufa huku akikwangua udongoni.* Usiivunje heshima ya mama yako.

Kutokana na mifano hii miwili, ni wazi kwamba mtafsiri aliipotosha maana ya methali hizo kimatumizi na kuathiri mtindo wa mwandishi ambao ndio sanaa yake. Katika methali ya kwanza, Tinka anashindilia mwanawe uovu wa Wamala, kwamba si lolote si chochote. Kaija anajua kwamba babake Wamala alikuwa mtu wa maana na cheo hapo awali, na kwamba daima Wamala hulalamika kuwa Tinka ndiye aliyesababisha kuporomoka kwake. Katika kujitoa katika lawama hii, Tinka anaeneza maneno yaliyojaa sumu kwa Wamala dhidi ya watoto wake. Methali ya "*A Lion is not a lamb*" inasisitiza haya.

Tinka ametumia methali ya pili akijirejelea mwenyewe. Anajaribu kwa kila namna kumdunisha Wamala kwa kuonyesha watoto kwamba baba yao hawajali kamwe. Kwamba ana wanawake wengine anaowajali zaidi na kazi yake muhimu ni kulewa kutwa kucha. Anajipendekeza kwa watoto ili wamchukie baba yao. Kulingana na muktadha wa methali hii, Tinka anajinasibisha na chui jike ambaye hatakaa chonjo na kuwaangalia watoto wake wakifanya kazi za

kujidunisha. Anachotaka kusisitiza Tinka ni kwamba kama si kwa sababu yake, watoto hawa wangekuwa washakufa kwa sababu baba yao hawajali. Methali hizi pia zinaeleza kwa undani zaidi tabia za Tinka ambazo toka mwanzo hadi mwisho wa tamthilia zinaonyesha mwanamke asiyeridhika, mwanamke ambaye haambiliki hasemezeki.

Ni wazi kwamba tafsiri ya methali hizo imepotoka. Mtafsiri alizitafsiri kwa njia ya moja kwa moja bila kujali muktadha wala athari ambayo methali hizi zingeleta kimaana. Matokeo yake ni kwamba, methali hizo hazina mnato wala ufasaha katika kazi tafsiri. Jambo hili limedhihirisha kwamba, matumizi ya methali za lugha pokezi au za kutafsiriwa moja kwa moja kuchukua nafasi ya methali fulani katika tafsiri mara nyingi huipotosha tafsiri. Tafsiri za methali hutaka uangalifu sana kwa sababu makosa ya kuzitafsiri vibaya hutokea zinapotafsiriwa moja kwa moja; bila kujali muktadha wa matumizi yake.

Mtafsiri hakutafsiri methali zote kwa njia ya moja kwa moja. Kuna methali ambazo alizingatia maana na muktadha na akazipa tafsiri mwafaka. Mfano ufuatao ni tafsiri nzuri ya methali aliyofanya mtafsiri.

Makala asilia UK 8

Kajia: *A promise is a promise*, you always say.

Makala pokezi UK 8

Kajia: *Ahadi ni deni*, ndivyo usemavyo kila mara.

Mtafsiri katika sehemu hii alitumia methali ya Kiswahili ambayo inafungamana na muktadha na ambayo ina maana sawa na ile ya kazi asilia.

Hata hivyo, kuna methali nyingine ambazo Muro alizifasiri badala ya kuzitafsiri. Kufasiri

methali kuna hatari ya kupotosha maana kama vile kuitafsiri kwa njia ya moja kwa moja. Inapofasiriwa, methali huwa si methali tena bali fungu la maneno ambalo halina umuhimu. Mtafsiri alifanya makosa ya kufasiri hivi basi kufanya sanaa ya mwandishi kuwa hafifu. Kuna mifano ifuatayo;

Makala asilia UK 23

Wamala: ...They're bent on sucking the blood out of us until we drop dead.

Tinka: *Bleeding a leech to fatten a heifer.*

Makala pokezi UK26

Wamala: Ninakwambia hii hi anasa na ni unyonyaji moja kwa moja. Wamepania kutunyonya mpaka tuwe wakavu hatuna damu; tufilie mbali.

Tinka: *Kumnyang'anya asiyekuwa nacho na kumpa aliye nacho.*

Makala asilia UK 43

Tinka: Some Yankee secretary or other will hung up.

Wamala: A Yankee secretary! These bastards know the game.

Tinka: *Trusting a black lamb to a white lioness.*

Makala pokezi UK 47

Tinka: Hiyo simu inaweza kukatwa na karani Mmarekani yoyote.

Wamala: Karani Mmarekani! Washenzi hawa wanazijua mbinu zote.

Tinka: *Ni kama kumchukua kondoo na kumpa simba amtunze.*

Kutokana na mifano hii, mtafsiri hatambui kwamba kuna tofauti kati ya tafsiri na fasiri. Hatuhitaji mjadala mrefu kuonyesha kuwa tafsiri hii haijapotoka tu bali pia imeua sanaa ya mwandishi. Katika mfano wa kwanza "*bleeding a leech to fatten a heifer*", mwandishi

anamulika kwa darubini kali sana uozo ulio katika jamii anayoizungumzia. Anaonyesha jinsi unyonyaji umeganda katika jamii haubanduki. Mtafsiri anapotumia neno kunyang'anya katika fasiri yake, anatupa maana ya juu juu tu. Unyonyaji anaoashiria mwandishi hauna kifani. Kwa mtafsiri kufanya kosa hilo, hakuathiri sanaa ya mwandishi tu bali pia maudhui na hulka za wahusika.

Mfano wa pili, "*Trusting a black lamb to a white lioness*" unaonyesha udhalimu wa wamerakani dhidi ya waafrika. Waafrika wamedhulumiwa kiasi kwamba hawana haki yoyote. Kulingana na muktadha wa matumizi, karani mmarekani analipwa kuzuia mwafrika kumfikia anayetaka. "Black lamb" inaashiria unyonge ilhali "white lioness" inaashiria uhodari na nguvu za Mmarekani. Kazi tafsiri haitoi maudhui haya jinsi hiyo. Kwa kutotafsiri methali hiyo vilivyo, mtafsiri amebana maudhui ya kazi nzima. Angefanikiwa kama angetumia na kuzingatia maana katika kazi yake.

### 3:4:2 TAFSIRI ZA NAHAU

Kwa Mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981), nahau ni fungu la maneno ambayo yakipangwa pamoja huleta maana isiyo ya kawaida ya kuonekana wazi. Mwandishi wa *The Burdens* ametumia lugha ya kinahau. Nahau hizi zimetafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja au zikapotoshwa katika makala tafsiri. Kuna mifano maridhawa kuthibitisha haya. Kwa mfano katika mwanzo wa mchezo *The Burdens*, mandhari tunayokutana nayo ni ya hali ya umaskini katika familia fulani. Maelezo yanasema hivi;

Makala asilia UK 1

> "Tinka is sitting alone, weaving a mat. Passing time? Waiting for Wamala? She wears an *I have been through hell* kind of face..."

Makala pokezi UK 1

> "Tinka amekaa peke yake akisuka mkeka. Anapitisha muda? Anamngojea Wamala? Uso wake unaonyesha *hali ya huzuni na uchovu wa maisha...*"

Tofauti na tanzu nyingine za kifasihi, tamthilia huwa na maelezo ambayo yanamwandalia msomaji au matazamaji mandhari ambayo mchezo unaigiziwa. Maelezo haya pia huonyesha hali ya wahusika walio jukwaani hivi kwamba hata kabla ya mchezo wenyewe kuanza, mtazamaji au msomaji ana picha kamili ya yale yatakayofuatia, na pia ana picha ya hali ya wahusika na namna ya maisha yao. Maelezo haya huwa nia yake ni kuarifu wasomaji na watazamaji watakachokitarajia katika onyesho hilo.

Katika kutuandalia mandhari ya onyesho la kwanza, mwandishi amefaulu kutuonyesha hali ya jamii hiyo, na hali ya mhusika Tinka aliye jukwaani wakati huo. Mwandishi alitumia neno "hell" kusisitiza hali ya maisha ya mhusika Tinka. Ni hali ya maisha yaliyojaa taabu nyingi. Anatutayarishia mhusika ambaye tutakutana naye katika tamthilia nzima, ambaye huenda ikawa tabia yake imechangiwa na hali yake ya maisha. Neno lile "hell" lina uzito sana likilinganishwa na tafsiri ambayo inasema kuwa Tinka yuko katika hali ya huzuni na uchovu wa maisha. Ni kana kwamba kulingana na tafsiri, Tinka amekata tamaa. Tafsiri hii inajikita katika hali ya sasa ya mhusika na wala haielezi hali ya hapo awali ya mhusika huyu. Mtafsiri hana uwezo wa kuichezea lugha kama afanyavyo mwandishi . Mtindo wa mwandishi ulimshinda kutafsiri na ni hali ambayo imeathiri lugha ya kazi tafsiri.

Kuna mifano zaidi ya aina hii;

Makala asilia UK 6

> Kajia: · Then he said sadly, "You don't have to say anything son... I can

tell the kind of poison she spreads against me. But remember. *She dragged me down*".

Makala pokezi UK 7

Kajia: Halafu alisema kwa huzuni, "Si lazima useme mwanangu... Najua sumu anayoieleza. Lakini - kaa ukikumbuka. *Aliniangusha*.

Makala asilia UK 10

Kajia: Wonderful times (sits down) with my grandfather?

Tinka: Oh.. Not a bad father really... but *men are mean son*. The only times they seem really happy is when they are outside their homesteads.

Makala pokezi UK 11-12

Kaija: Ukifurahi (anakaa) na babu yangu?

Tinka: Kusema kweli hakuwa baba mbaya lakini *wanaume ni choyo mwanangu*. Wakiwa nje ya nyumba zao ndipo wanapokuwa na furaha.

Mtafsiri alitafsiri nahau hizi kwa njia ya moja kwa moja hivi basi akapotosha lugha. Neno "mean" katika Kizungu linaweza kuchukua maana mbalimbali kutegemea muktadha wa matumizi. Kwa kulitafsiri neno hilo kwa njia ya moja kwa moja, mtafsiri ameipotosha nahau hiyo na haitokei kama nahau katika makala pokezi. Mtafsiri ametumia neno "mean" kuwa choyo. Ingawa choyo ni maana moja ya "mean", mwandishi hakukusudia choyo katika makala asilia. "Mean" pia inaweza kuwa na maana ya kadiri, wastani, bahili, choyo ama kujipenda. Katika muktadha wa kazi asilia, neno hili linamaanisha kujipenda, kwamba wanaume wanajipenda sana. Kwamba wao wanapata raha huko nje na wanawake wengine

lakini wakirudi nyumbani huwa wamenuna. Mtafsiri hakuzingatia muktadha wa neno hilo. Kutumia neno choyo kwa maana ya "mean" kunaleta maana ya mtu anayenyimwa kitu fulani. Kama mtafsiri angezingatia maana angekuwa na tafsiri bora zaidi.

Kwa kutumia "she dragged me down" katika mfano wa kwanza, Wamala anamwambia mwanawe kuwa Tinka alisababisha kuporomoka kwake ki - hali na mali. Kuwa Tinka hakumsaidia katika lolote ila tu kuharibu heshima yake. Katika tafsiri, mtafsiri anatumia neno 'aliniangusha' ambayo haileti maana aliyokusudia mwandishi. Mwandishi hakulitafuta neno mwafaka ambalo lingefaa katika nahau hii. Angetumia neno linaloonyesha kusababishwa kwa kushuka cheo kwa Wamala na Tinka.

### 3:5 TAFSIRI ZA MOJA KWA MOJA

Katika tafsiri yoyote, inambidi mtafsiri kuelewa kazi anayoishughulikia kabla ya kuanza kazi ya kutafsiri. Ili kuepuka tafsiri iliyopotoka, inabidi pia mtafsiri ajiepushe na tafsiri za moja kwa moja kwa sababu kama tulivyosema hapo awali, tafsiri hizi huegemea upande mmoja na mara nyingi hazina maana yoyote katika tafsiri. Tafsiri ya moja kwa moja huwa haina maafikiano. Fauka ya tafsiri ya moja kwa moja kuelemea katika lugha ya makala asilia, pia huelemea upande wa mawazo ya mwandishi wa makala hayo. Ijapokuwa tafsiri hukusudiwa msomaji katika lugha pokezi, tafsiri za moja kwa moja hazina manufaa kwa msomaji huyo.

Kwa sababau ya tofauti nyingi, hasa maana katika lugha za Kilimwengu, tafsiri za moja kwa moja hupotosha maana ya lugha pokezi. Tafsiri hizi zina dosari nyingi kwa sababu hakuna lugha mbili za ulimwengu zinazoafikiana kimaana. Tumesema kwamba kuna maneno ambayo yanaweza kubeba maana mbalimbali kutegemea muktadha wa matumizi. Kuyapuuza mambo

kama haya husababisha kufinywa kwa maana na thamani ya neno katika lugha pokezi. Isitoshe tafsiri za moja kwa moja huleta mgongano kati ya lugha mbili tofauti. Zinaweza tu kukadiria maana lakini haziwezi kupata wiano kamili. Kuna mifano ya kutosha kuonyesha kwamba mtafsiri alitumia njia ya moja kwa moja kuitafsiri kazi ya *Mizigo*. Tayari tumetoa mifano ya methali na nahau. Ifuatayo ni mifano zaidi inayoathiri tafsiri nzima.

Mwandishi ametumia neno "old" kuonyesha upendo na kusifu. Ni mhusika Wamala ambaye analitumia neno hili kumsifu mkewe na mwanawe na pia kuwabembeleza. Kwa sababu ya tafsiri za moja kwa moja, tafsiri hizi zimejitokeza kama matusi. Kwa mfano;

Makala asilia UK 18

Wamala: How is the *old girl* tonight?...

Come on *old girl*. Like to feel it's comfort?

Tinka: (Not looking up from her weaving) We are fed up with second-hand things.

Wamala: Come on Tinka, don't be nasty. The bed's still in reasonable condition. Strong and comfortable. Bet it'll excite the *old boy* out of his senses.

Makala pokezi UK 20

Wamala: U hali gani *mzee wa kike*?... *Njoo mwanamke*. Unataka kuihisi raha yake?

Tinka: (Bila ya kuinua macho) Tumechoka na vitu vikuuvikuu.

Wamala : Wacha matata Tinka. Hiki kitanda bado kina hali nzuri. Ni madhubuti. Kitamfurahisha *bwana mdogo* wetu.

Tukirejelea mifano hii, ni dhahiri kwamba tafsiri za moja kwa moja hupotosha tafsiri kwa kiasi

kikubwa kimaana. Kulingana na kazi asilia, Wamala anajaribu ujanja wowote kumfurahisha mkewe ambaye daima hakidhiki. Anamwita mkewe "old girl" kumhadaa. Kwa sababu yatafsiri ya moja kwa moja, maneno haya hayapendezi katika kazi pokezi. Ni kama Wamala anamkemea na kumuamrisha mkewe.

Mtafsiri alifanya jambo la busara kutafsiri "old boy" kuwa bwana mdogo. Jina hili ni la kubembeleza na mwandishi pia alinuia jina hili liwe la kupendeza kwa Kajia. Katika sehemu hii mtafsiri hakutumia tafsiri ya moja kwa moja. Badala yake alizingatia maana ambayo ni muhimu katika tafsiri yoyote.

Tafsiri ya moja kwa moja ambayo imefanya kazi tafsiri tofauti kabisa na kazi asilia inajitokeza katika;

Makala asilia UK 38

| | |
|---|---|
| Wamala: | Do you know why I found it particularly exciting? |
| Tinka: | Curiosity. That's all. |
| Wamala: | *The pleasures behind the habit*? |

Makala pokezi UK 41

| | |
|---|---|
| Wamala: | Unajua ni lipi hasa lililonisisimua? |
| Tinka: | Udaku tu, basi. |
| Wamala: | *Raha ya tabia hiyo*? |

Tafsiri hii haina uhusiano wowote na yaliyomaanishwa katika kazi asilia. Tunakariri tena kwamba kuna maneno yaliyo na zaidi ya maana moja katika kila lugha. Ni muhimu kwa mtafsiri kuzingatia umuhimu wa maana ya kila neno kabla hajaanza kutafsiri. Mwandishi

alitumia neno "habit" kwa maana ya vazi la kidini linalovaliwa na watawa. Kulingana na muktadha wa mazungumzo, Wamala na Tinka wanakumbuka kukutana kwao wakati ambapo Tinka alikuwa mtawa naye Wamala mwanasiasa. Wamala anamwambia Tinka namna alivyokuwa na hamu ya kujua ni nini kilichofichika ndani ya vazi hilo ambalo watawa huvalia wala hazungumzii juu ya tabia yoyote kama mtafsiri anavyodai. Kwa sababu ya kutozingatia maana mtafsiri amejitokeza na tafsiri mbovu iliyo na makosa mengi, iliyokosa usahihi na inayodhoofisha sanaa ya mwandishi si haba.

Mbali na makosa ya tafsiri za moja kwa moja, mtafsiri amefanya tafsiri zisizo sahihi ambazo zimeleta tofauti kubwa kimaana na kazi asilia. Inaelekea kwamba mtafsiri hakusoma kazi anayoishughulikia kwa kituo na aliitafsiri kabla ya kuelewa. Huenda pengine hakuuelewa mtindo wa mwandishi na kwa sababu hiyo akaupuuza au akaubadilisha kimakusudi, jambo ambalo ni makosa kufanya kwa sababu mtafsiri anapaswa kuwa mwaminifu kwa mwandishi. Kwa kufanya hivi, mtafsiri ameuathiri mtindo wa mwandishi na pia sanaa ya kazi asilia kwa kiwango kikubwa.

Mtafsiri huenda akakosa visawe vya maneno fulani katika lugha tafsiri, lakini makosa haya yanapojitokeza kwa wingi na hasa yanapohusiana na sanaa ya mwandishi, hayana budi kuonyeshwa na kujadiliwa. Kuna mifano maridhawa ya makosa kama haya yanayojitokeza katika tafsiri ya *Mizigo*. Mengi ya makosa haya yamejitokeza pale mtafsiri anapojaribu kuepuka lugha zenye makali au matusi ya mwandishi. Kwa mfano:

Makala asilia UK 10

Kaija: I Wish father was here now.

Tinka: Ask his other women why he isn't (to herself). Thinks *tarts and*

*beer tubes* will solve his problems.

Makala pokezi UK 11

Kaija: Natamani lau baba angekuwa hapa nyumbani sasa.

Tinka: Waulize wake zake kwa nini mpaka sasa hajafika (anajiambia mwenyewe). Anafikiri *mirija na vileo vyake vikali* vitamtatulia matatizo yake...

Mwandishi anatumia neno "tart" kumaanisha malaya. Tinka kama kawaida anaeneza ubaya wa Wamala kwa watoto wake, kwamba ana wanawake wengine ambao anawathamini zaidi kuliko mkewe (Tinka). Ni kawaida ya wanawake wengi kuwaita wanawake ambao wana uhusiano na waume wao malaya hata ikiwa uhusiano huo si wa kimapenzi. Mtafsiri analitafsiri neno hili kuwa vileo vikali. Neno hili lina maana hiyo pia lakini sio muktadha wa mazungumzo haya.

Makala asilia UK 24

Wamala: She looked at my tattered jacket with scorn, pulled out a 'HAKUNA KAZI' poster, and sweetly said the managing director was busy. And all the time *the bugger was there scratching his balls*. I told her I wasn't looking for a job. She said I was becoming a nuisance...

Makala pokezi UK 26

Wamala: Aliyaangalia matambara yangu kwa dharau, akavuta dawati lake na kutoa tangazo lililoandikwa 'HAKUNA KAZI' na akaniambia kwa sauti nyororo kuwa mkurugenzi msimamizi ana shughuli nyingi. Na hali wakati huo wote mkurugenzi alikuwa ndani wala hana kazi *Maalumu*. Nilimwambia msichana huyo

kuwa sikuwa na haja ya kazi...

Huu ni mfano mwingine unaoonyesha tafsiri isiyo sahihi. Mwandishi alidhamiria kuonyesha utumiaji mbaya wa wakati na mamlaka mtindo ambao ni wa kawaida kwa watu wenye vyeo. Mtafsiri kusema 'wala hana kazi maalumu' ni kama kuonyesha alikuwa na kazi fulani nyingine. Mwandishi alitaka kusisitiza uzembe wa mkurugenzi huyo, na namna Wamala anavyodhulumiwa kule ofisini mwake. Kwa kutumia maneno yaliyojaa matusi, mwandishi anaonyesha dharau na bezo kwa wakurugenzi hawa ambao badala ya kuhudumia taifa, wanakaa bure ofisini. Isitoshe, wana makarani na walinzi ambao wanazuia watu wasiwafikie. Kwa mtafsiri kuepuka lugha ya mwandishi, amefanya maudhui ya makala pokezi kuwa dhaifu. Fauka ya hayo, sanaa ya mwandishi imekuwa hafifu.

**3:6 UMBUJI WA MWANDISHI KATIKA TAFSIRI**

Mwandishi wa *The Burdens*, John Ruganda ni mwandishi ambaye ana uwezo wa kutumia lugha kwa njia isiyo ya kawaida. Katika mtindo wake, mwandishi huyu hubuni istilahi za aina ya kipekee za matumizi ya lugha. Mtindo huu huweza kuikuza sanaa yake.

*The Burdens* ni tamthilia ambayo imeandikwa kwa ufundi mwingi kifasaha. Mwandishi amebuni msamiati mwingi ili kuitia lugha yake madaha. Msamiati huu umefanya tamthilia nzima kuwa ya hali ya juu kisanaa. Mtafsiri alishindwa kuutafsiri msamiati huo na kuhifadhi sanaa ambayo mwandishi alitumia kimadaha. Mtafsiri pia ameifasiri na mara nyingine anatafsiri kile anachofikiria mwandishi alitaka kumaanisha. Kwa kufanya hivi, mtafsiri ameinyima kazi tafsiri ladha kisanaa.

Waandishi wengi hutumia maneno ya lugha yao ya kwanza kusanii kazi zao. Mwandishi

ametumia maneno ya lugha ya Luganda hapa na pale. Ni vizuri mtafsiri kuyaacha maneno kama haya bila kuyatafsiri. Mtafsiri wa *Mizigo* ameyaacha maneno mengi ya lugha ya Luganda kama hayajatafsiriwa. Hata hivyo, ametafsiri baadhi yake kama vile 'kondo' ambalo ni jina aliyoipa kisawe cha majambazi na 'Enguli' jina ambalo amelipa kisawe cha chang'aa. Sababu za mtafsiri kuyatafsiri baadhi ya maneno na kuyaacha mengine haieleweki moja kwa moja, lakini jambo moja ni wazi kwamba, kwa kufanya hivi ameathiri sanaa ya mwandishi. Mwandishi pia ametumia jina "Kill me quick" kumaanisha pombe hiyo hiyo "Enguli". Mtafsiri kwa upande wake ameipa kisawe cha chang'aa.

Makala asilia UK 28-29

| | |
|---|---|
| Wamala: | Is your '*kill me quick*' sold out? |
| Tinka: | (To distract him) Yes. |
| Wamala: | Half a bottle will do. People praise your *enguli* as the best in the slums.... A quarter of '*kill me quick*' would spin it out more quickly though. |

Makala pokezi UK 31-32

| | |
|---|---|
| Wamala: | Umemaliza kuuza *chang'aa* yako? |
| Tinka: | (Ili kumpambaniza) Ndiyo. |
| Wamala: | Nusu chupa tu itanitosha. Watu wanaisifu *pombe* yako ya kuwa ni nzuri kupita zote zinazouzwa.... Robo chupa ya *chang'aa* ingenisaidia kueleza upesi zaidi wazo lenyewe. |

Katika makala asilia, inaelekea kuwa jina 'enguli' lina maana ya chang'aa. Sababu ambayo ilimfanya mtafsiri kutafsiri 'kill me quick' kuwa chang'aa na 'enguli' kuwa pombe haieleweki. Isitoshe, jina "kill me quick" alilotumia mwandishi linaipa pombe hiyo uzito na athari zinazohusishwa nayo. Sio kwamba mtafsiri angetafsiri neno kwa neno ili kuleta maana na

uzito huu, lakini jina chang'aa linaipa pombe hiyo sifa hafifu ikilinganishwa na 'kill me quick'. Pia jina chang'aa lina uwazi mno na mwandishi hakukusudia uwazi huo.

Makala asilia UK 35

Wamala: ...the world outside is hell let loose. It breaks one. Everyone orders you to walk with your *tail limp between your thighs*. They don't want you to raise your head.

Makala pokezi UK 38

Wamala: ulimwengu unaotuzunguka umejaa mateso. Hauna huruma. Unamvunjavunja mtu. Kila mmoja anakuamuru *uinamishe kichwa unapokwenda*. Hawataki uinue kichwa.

Labda kwa sababu ya kule kuchelea kutumia maneno makali ya mwandishi, hapa tena mtafsiri hakuzingatia umbuji wa mwandishi. Jambo hili limesababisha kutojitokeza kwa ulimwengu anaozungumzia mwandishi, ulimwengu ambao ni wa mwenye nguvu na ambao makabwela hawana nafasi. Tafsiri hii haiathiri sanaa ya mwandishi tu bali pia maudhui aliyokusudia mwandishi. Kuna mifano zaidi ya umbuji wa mwandishi ambao umedhoofishwa au kutafsiriwa vibaya.

Makala asilia UK 18

Tinka: There are some homes which have never known secondhand...

Wamala: And there are others that can't afford even *tenth hand* things, for your information.

Makala pokezi UK 20-21

Tinka: Kuna nyumba nyingine ambazo hazijapata kuwa na vitu vikuukuu isipokuwa vipya vitupu.

Wamala: Na ufahamu kuwa kuna nyingine ambazo hata *vikuukuu*

*vilivyochakaa* hazina.

Katika sehemu hii, mtafsiri amefanya nyongeza ambayo haipo katika makala asilia. Ile sehemu mhusika Tinka anayosema "...isipokuwa vipya vitupu" inapatikana katika makala pokezi tu lakini haipo katika makala asilia. Tumetaja kwamba mtafsiri hafai kufanya zaidi ya tafsiri. Ni sharti awe mwaminifu kwa mwandishi. Mtafsiri hapa anaikuika sheria hii na kufanya kinyume.

Huenda ikawa kwamba mwandishi alitaka kuonyesha tabia ya Tinka ya kumdunisha mumewe. Sio lazima aongezee mambo mengine ili tabia hii idhihirike. Kwa kweli katika sehemu hii, Tinka anataka kumkumbusha Wamala kwamba hawezi kuikimu familia yake. Anachoweza kununua ni vitu ambavyo tayari vishatumiwa. Wamala katika kujitetea kwake anatumia usemi "tenth hand" kumaanisha kuwa kuna familia ambazo ni maskini kuliko yao. Usemi huu 'tenth hand' unatupa uwezo wa mhusika Wamala wa kubuni lakini tafsiri ya 'vikuukuu vilivyochakaa' haionyeshi ubunifu wowote.

Sio kwamba mifano tuliyotoa ndiyo umbuji wa mwandishi tu, umetamba kote katika kazi hii. Tumeonelea kuwa ni muhimu kutoa mifano ya hapa na pale. Mtindo wa mwandishi kwa jumla ni wa ustadi mwingi.

## 3:5 TAFSIRI ZA SITIARI NA TASHBIHA

Tashbiha na sitiari ni njia ya kitamathali ya kulinganisha kitu kimoja na kingine. Ambapo sitiari hulinganisha vitu bila kutumia viunganishi kama vile kama, mithili ya, n.k; tashbiha huvitumia. Tamathali hizi za lugha hutumiwa na waandishi wengi kuzisanii kazi zao. Ruganda anatumia tamathali hizi kwa wingi na kufanya kazi yake *The Burdens* ipendeze kisanaa.

Ni kweli kwamba sitiari na tashbiha ni ngumu kutafsiriwa kwa sababu huenda ikawa kwamba visawe vya vitu vinavyolinganishwa katika kazi asilia haviko katika lugha pokezi. Katika *Mizigo* kuna sitiari na tashbiha nyingi ambazo zimetafsiriwa moja kwa moja, jambo ambalo limesababisha tamathali hizi zisionekane kama tashbiha au sitiari tena. Nyingine zimebadilishwa na badala ya kutafsiriwa kama sitiara zimejitokeza kama tashbiha, na tashbiha kama sitiara. Kuna mifano inayoonyesha kubadilishana huku kwa nafasi;

Makala asilia UK 6

| | |
|---|---|
| Tinka: | That's what he tells you. |
| Kaija: | That you kept pulling hin down and down. *A millstone round his neck* he says. *A big burden.* |

Makala pokezi UK 7

| | |
|---|---|
| Tinka: | Hayo ndiyo anayokwambia. |
| Kajia: | Kwamba kila kukicha ulikuwa ukiendelea kumvuta chini. Kuwa ulikuwa *jiwe la kusagia lililofungwa shingoni mwake.* |

Katika mfano huu, mtafsiri hakuitafsiri jazanda moja ambayo imebeba uzito wa sehemu hii yote. Mwandishi alimalizia sehemu hii na jazanda ya "a big burden" ili kusisitiza ile ya kwanza ya jiwe la kusagia lililofungwa shingoni. Tafsiri ya 'a big burden' haipo. Tamthilia yote ni jazanda tupu. mzigo mzito zaidi uliombidi Wamala aubebe ni Tinka ambaye kila wakati

alimlemea. Kwa kutoitafsiri sehemu hii, dhamira ya tamthilia tafsiri imekuwa hafifu. Tabia ya Tinka pia haijitokezi kama inavyojitokeza katika kazi asilia.

Jazanda nyingine ambayo inaelezea tabia ya Tinka na ambayo ilifasiriwa badala ya kutafsiriwa iko katika:

Makala asilia UK 75

Kaija: "...only remember, life is not easy when you have a *slob of a woman* always dragging you down and *spreading poison* against you."

Makala pokezi UK 80

Kaija: "...isipokuwa ukumbuke kuwa maisha huwa si mazuri uwapo na mwanamke ambaye *anauma na kupuliza*, kila siku anakuvuta chini na *kukutilia sumu*."

Mazungumzo haya ni baina ya Kaija na mamake Tinka. Kaija anamueleza mamake yale aliyoambiwa na Wamala kuhusu Tinka. 'Slob' ambayo ndiyo Wamala analinganisha Tinka nayo ni mjinga mkubwa. Katika tafsiri, mtafsiri anasema kuwa Tinka ni mwanamke wa kuuma na kupuliza. Haya si kweli. Tinka anauma, lakini hapulizi hata mara moja. Kwa kutozingatia maana aliyokusudia mwandishi, mtafsiri amejitokeza na tafsiri mbaya ambayo haielezi yale ambayo mwandishi ameandika. Mtafsiri pia ametafsiri 'spreading poison' kuwa kutilia sumu. Mwandishi alimaanisha kuwa Tinka anaeneza mambo mabaya juu ya Wamala, wala hakumaanisha kuwa alimtilia sumu. Kuwa na tafsiri ambayo si sahihi kumefanya kazi tafsiri kuwa ya kiwango cha chini kisanaa. Mtafsiri hakutilia maanani maana ambayo mwandishi alikusudia na ndiyo sababu aliibuka na tafsiri ya aina hii, tafsiri iliyokosa ladha ya kazi asilia.

Mifano zaidi tunaipata katika:

Makala asilia UK 35

Wamala: You provoked me. Shouldn't have treated me like that. A man always wants a little bit of respect.... To make him feel he is the boss in his house, not a *door-mat for every bastard to wipe his shoes on....*

Makala pokezi UK 38

Wamala: Wewe ndiye uliyenichokoza. Hungenitenda kama ulivyonitenda. Mwanamume anataka apewe heshima japo kidogo tu, ...na wala si *kama kirago cha mlangoni cha kufutia viatu vya kila mbwa anayeingia.*

Zaidi ya kuibadilisha sitiara ya kazi asilia kuwa tashbiha katika kazi tafsiri, mtafsiri anarudia makosa ya kufanya zaidi ya tafsiri. Mtafsiri anatafsiri jina la 'bastard' kuwa mbwa na kufanya hivi ni kuongeza mambo ambayo hayako katika kazi asilia. Sababu ya kufanya nyongeza hii si wazi. Huenda ikawa mtafsiri alitaka kutumia jina linalokera kama alivyofanya mwandishi. Hata hivyo, jina 'mwanaharamu' lingekuwa neno mwafaka kwa tafsiri ya 'bastard' na pia jina hilo linakera. Inaelekea kwamba mtafsiri alishindwa kuitafsiri sanaa ya mwandishi hivi basi akapotosha mtindo na maana iliyokusudiwa na mwandishi.

Kwa upande wa tashbiha, mtafsiri pia hakuzitafsiri na kuzitoa kama zinavyojitokeza katika kazi asilia;

Makala asilia UK 67

Kaija: Didn't he come back last night ... from the Republic?

Tinka: He did, *wet as a sponge*, but he's gone.

Makala pokezi UK 74

Kaija: Hakurudi usiku wa jana ... kutoka 'Jamhuri'?

Tinka: Alirudi akiwa *amelewa sana* lakini sasa ametoka.

Katika mfano huu tunaona namna tashbiha ilivyofasiriwa katika kazi tafsiri. Mtafsiri aliyafasiri yale ambayo yamo katika kazi asilia. Kukosa kuitafsiri tashbiha hii, mtafsiri amewanyima wasomaji taswira ambayo mwandishi aliikusudia kutoa picha ambayo ni ya Wamala aliyelewa chakari, picha ya mtu aliyetota kwa pombe.

Sio sitiari na tashbiha tu ambazo ziliathirika katika tafsiri ya *Mizigo*. Tamathali nyingine kama vile tashihisi, maswali ya balagha na takriri hali kadhalika hazikutafsiriwa kitamathali kwa mfano makala asilia UK 20 Wamala anamwambia Tinka "*A limousine is beckoning*". Katika kazi tafsiri *Mizigo*, Wamala anamwambia Tinka "*kuna dalili za kupata gari mpya*". Mwandishi alitaka kuonyesha ndoto za Wamala ambaye kila siku alitamani maisha ya utajiri na raha kama hapo awali. Katika mazungumzo haya, Wamala anamwambia Tinka kuwa gari mpya linawakonyeza, linawaita walimiliki. Katika tafsiri mtafsiri ameipotosha maana hiyo kwa kusema kuna dalili. Katika ndoto zake Wamala hakuona dalili yoyote bali ukweli kwamba atalipata gari hilo na vyote alivyopoteza hapo mbeleni.

Huu ni mfano mmoja wa yale mtafsiri aliyopotosha katika kutafsiri tashihisi alizotumia mwandishi. Mbali na mfano huu, kuna mambo ambayo mtafsiri aliingiza katika tafsiri ili aweze kujieleza. Kwa kufanya hivi, mtafsiri alipotosha maana ya tafsiri basi iliathirika kisanaa na kimaudhui.

## 3:6 HITIMISHO

Katika sura hii tumeonyesha na kujadili dosari na makosa ambayo yanafanya kazi ya *Mizigo* kuwa dhaifu kisanaa. Tumeonyesha mifano ya makosa haya aliyofanya mtafsiri. Pia tumezitaja sababu zilizosababisha udhaifu huo. Baadhi ya sababu hizo ni kama vile kutoelewa lugha ya mwandishi, kutoielewa mifumo ya umbuji na uelezaji na kutozingatia maana katika tafsiri. Tasnifu hii inaonelea kwamba kutozingatia maana katika tafsiri yoyote ni sababu moja kubwa inayosababisha udhoofishaji uliofanywa katika *Mizigo*.

Kama tulivyoonyesha, mtafsiri alitumia sana tafsiri za moja kwa moja bila kuzingatia matokeo yake. Pia mtafsiri alikiuka sheria za tafsiri. Alifanya nyongeza na kupunguza mambo muhimu katika kazi asilia, jambo ambalo lilifanya mtafsiri ashindwe kuwasilisha kazi asilia katika lugha na maana yake. Kufanya hivi pia kumeinyima kazi tafsiri sifa na nguvu zake za kifasaha.

Makosa mengine yaliyofanyiwa kazi pokezi ni upotoshi wa lugha. Mtafsiri alipuuza au hakuelewa mtindo wa matumizi ya lugha ya mwandishi. Mtafsiri aliondoa matumizi ya lugha ya kitamathali na akautoa ladha umbuji wa mwandishi. Lugha iliyokuwa na makali na ucheshi katika makala asilia haipo katika kazi tafsiri. Bi Muro alitafsiri mtiririko tu na kuacha mambo mengi yanayohusu lugha na zile mbinu nyingine zinazoifanya kazi asilia kuwa ya sanaa. Mtafsiri alipuuza mtindo, umbuji na muktadha. Mtafsiri hahitaji kutafsiri yaliyomo tu bila kuzingatia yale yote yanayoifanya kazi kuitwa ya kifasihi. Maadamu makosa haya yote yanajitokeza katika kazi hii, tunasisitiza kwamba *The Burdens* haikumfikia msomaji wa Kiswahili katika ufasaha wake.

## TANBIHI


1. Zaja O. (1986)
   *Fasihi Tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili: matatizo na athari zake.* Tasnifu ya M.A. Nairobi.

2. Msokile M. (1993).
   *Misingi ya uhakiki wa fasihi.* East African Educational Publishers Ltd. Nairobi.

3. Wellek R. & Warren A. (1949).
   *Theory Of Literature.* Janathan Cape. Great Britain.

4. Ngara E. (1985).
   *Art and Ideology In The African Novel.* Heineman Educational Books, London.

5. Lefevere A. (1975).
   *Translating Poetry.* Van Gorcum, Assen Amsterdam, The Netherlands.

6. Newmark P. (1982).
   *Approaches To Translation.* Pergamon Press.

7. Crystal D. & Davy (1969).
   *Investigating English Style.* Longman, London.

8. Leech K. M. & Short L. M. (1981).
   *Style In Fiction*, Longman, London.

SURA YA NNE

## 4:1 HITIMISHO

Katika tasnifu hii, utafiti umefanywa juu ya sanaa katika fasihi tafsiri. Shabaha muhimu ilikuwa ni kuonyesha mambo yanayochangia, kuathiri na kusababisha makosa ambayo nayo pia yanaathiri lugha na mtindo katika makala pokezi. Tumejaribu kuonyesha athari zinazotokana na mtafsiri kutozingatia muktadha ambao lugha imetumika. Ukwasi wa mtasfsiri wa kiisimu, kilugha na kifasihi huchangia katika kuamua aina na kiwango cha tasfsiri anayofanya. Mtafsiri akishindwa na kuyathibiti hayo tuliyotaja hapo juu, kazi yake haina budi kuwa na udhaifu fulani.

Kutokana na utafiti wetu, tumeona ya kuwa ulinganifu wa makala asilia na makala pokezi huathiriwa sana na tofauti za miundo ya lugha zinazotofautiana. Kila lugha ina muundo wake wa kipekee na sheria zake tangu fonolojia, mofolojia na sarufi. Pili, tafsiri huathiriwa na tofauti za kimazingira na kitamaduni. Haya husababisha tofauti za kimaana na kifalsafa kwa sababu yote hufungamana na utamaduni maalumu. Matatizo ya kimaana yanayotokana na utamaduni pale ambapo pana tofauti katika miundo ya jamii na vifaa vya jamii husika.

Tumeonyesha katika tasnifu hii kwamba, mtafsiri anapokosa kuelewa dhamira ya makala asilia, kuelewa wajibu wake katika tafsiri na asipokuwa na utaalamu wa kazi inayotafsiriwa, bila shaka kutatokea dosari katika tafsiri. Huenda pia tafsiri isifue dafu. Hata hivyo, hutokea nyakati ambapo mtafsiri anakosa kisawe na hana budi kutokuwa mwaminifu kwa mwandishi. "Usaliti" wa aina hii wakati mwingine hauepukiki.

Katika uhakiki wetu wa *Mizigo*, tulionyesha dosari kama vile mtafsiri kupanua au kupunguza

sehemu au maneno mengine fulani katika kazi pokezi na kuingiza fasiri yake kuhusu mambo fulani. Tulitaja pia dosari nyingine kama kushindwa kutafsiri umbuji wa mwandishi, upotoshi wa maana, mtindo, umbo na mawasiliano katika kazi asilia. Ugumu hutokea pale ambapo mtafsiri atapanua au kupunguza kwa njia itakayopotosha ujumbe asilia. Hatima hii inaweza kuepukika iwapo mtafsiri atatilia maanani vipengele vyote, hasa muktadha kabla na wakati wa kufanya tafsiri kwa kuipitia mara kwa mara.

Misingi ya kinadharia tuliyoteua imekuwa ni mhimili mkuu wa kazi hii. Mipaka tuliyoweka na nadharia jumuishi tuliyoteua imetuwezesha kuangalia vipengele kadha vya yanayohusika katika shughuli ya kutafsiri. Imetuwezesha kuangalia maswala yanayohusiana na lugha na wingi wa matumizi yake; isimu na mtindo bila kukiuka malengo yetu na kwa njia ambayo imeangaza yanayofaa kutiliwa maanani na watafsiri na wahakiki wa tafsiri ili kukuza sanaa ya kutafsiri.

Tungependa kusisitiza kwamba, kuna haja ya kuipitia kazi ya tafsiri mara kwa mara ili kuiboresha. Hili si jambo la pekee kuhusu tafsiri kwa sababu maandishi katika sajili nyengine pia hupitiwa ili kuboreshwa.

Sanaa katika tafsiri ni kipengele kinachofaa kuchunguzwa kwa sababu huathirika katika mpigo wa lugha na jinsi ujumbe unavyopelekwa na kuathiri hadhira pokezi. Kwa kufanyiwa utafiti zaidi, ufahamu wa jumla ya sanaa ya kutafsiri utakuzwa. Tahakiki za tafsiri si lazima zishutumu udhaifu wa tafsiri tu. Zitachangia pia katika ukuzaji wa mbinu za kuboresha taaluma tafsiri kiutendaji na ukubalifu wa makala tafsiri katika jumla ya makala nyengine.

Maoni ya tasnifu hii ya jumla ni kuwa, ingawa wasomi husema kuwa tafsiri ni kama chakula

kilichotafunwa, tafsiri iliyoidhoofisha sanaa ya makala asilia ni kama chakula kilichotafunwa na ladha yake kuondolewa. Haya ni maoni ya kibinafsi na ni jambo linalohitaji kufanyiwa utafiti ili kuthibitisha madai ya tasnifu hii au kuyakana.

## MAREJELEO


Aik K. C. & Edmonds (1976).
*Critical Thinking.* Longman Singapore Publishers (Pte) Ltd. Singapore.

Ali C.W. (1981)
*The Problems of Translating From English into Swahili.* As exemplified by V.O.K. news items. M.A. Thesis (unpublished) University of Nairobi.

Ashe G.(1972)
*The Art Of Writing Made Simple.* Richard Clay & Co Ltd. London.

Bakari M. (1984)
*The State Of Art.* Katika Kiswahili Literature in the 19th Century. Dar es Salaam.

Beekman J. & Callow J. (1974).
*Translating The Word Of God.* Grand rapids,. Zondervan Publishing House. Michigan

Brower R.A. (Ed) (1966)
*On Translation.* Oxford University Press, New York.

Catford J.C. (1965).
*A Linguistic Theory of Translation.* Oxford University Press, London.

Chapman R. (1973).
*Linguistics And Literature.* Richard Clay Ltd. London.

Costello N. (1992)
*On Translation Theories.* Notes on Translation, Journal, TEXAS U.S.A.

Crystal D. & Davy D. (1969)
*Investigating English Style.* Dai Nippon Printing Co. International (Ltd), HONG-KONG.

Encyclopaedia Brittanica (1967).
15th ed. University of Chicago Press, Chicago.

Enkvist N.E. (1964).
*Linguistics And Style.* Oxford University Press. London.

Forster L. (1958).
'Translation: An Introduction' in *Aspects of Translation.* University of London Communication Research Center.

Harries L. (1970).
*Translating Classical Literature Into Kiswahili.* Katika Jarida la Chuo Cha

Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili (TUKI) Dar es Salaam.

Hermans T. (ed) (1985)
*The Manipulation of Literature: Studies in Literally Translation.* Groom Helm Ltd. Burrel Row Bekenham. Kent.

Hough G. (1973).
*An Essay on critisicim.* Reduced Press Ltd. Frowbridge Wiltshire G.B.

Kelly L.G. (1979).
*The True Interpreter. A History of Translation Theory and Practice in the West.* Basil Blackwell, Oxford.

Larson M.L. (1984).
*A Meaning Based Translation. A Guide to Cross Language Equivalence.* University Press of America.

Leech G.N. & Short M.H. (1981).
*Style in Fiction. A Linguistic Introduction into English Fiction Prose.* Longman Group, UK Ltd.

Lefevere A. (1975).
*Translating Poetry.* Van Gorcun Assen, Amsterdam.

Lodge D. (1966).
*Language of Fiction.* Routledge and Kegan Paul PLC, London.

Msokile M. (1993).
*Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* East Afrcan Educational Publishers Ltd. Nairobi.

Muro A. (1977).
*Mizigo. A translation of John Ruganda's The Burdens.* Oxford University Press, Nairobi.

Newmark P. (1988).
*A Text Book of Translation.* Prentice Hall International (UK) Ltd.

Ngara E. (1985).
*Art and Ideology in the African Novel.* Heinemann Educational Books Ltd. USA.

Nida E. (1964).
*Toward a Science of Translating.* E.J. Brill, Leiden, Netherlands.

Nida E. and Taber R.C. (1968).
*The Theory and Practice of Translation.* E.J. Brill, Leiden, Netherlands.

Rabin c. (Ed) (1958).
*Aspects of Translation.* University of London Communication Research Center, London.

Ruganda J. (1972). *The Burdens.* Oxford University Press, Nairobi.

Ryanga C.W. (1985).
*Vitabu Vya Kutafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili.* Katika Tuki Vol 52. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Sanders C.R. (1957).
*Lytton Strachey. His Mind and Art.* Oxford University Press / Yale University Press.

Shitemi N.L. (1990).
*Mawasiliano katika Tafsiri: Uteuzi wa Mtafsiri.* Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa) University of Nairobi.

Spencer J. & Gregory M. (1964).
*To the Study of Style.* Oxford University Press, London.

Thomas G. (1988). Notes on Translation. *Journal* Vol 2 No 1 texas, USA.

Widdowson H.G. (1975).
*Stylistics and the Teaching of Literature.* Hong Kong Group Ltd, Hong Kong.

Zaja O. (1986).
*Fasihi Tafsiri katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili.* Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa), University of Nairobi.